Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page i

# KUONEKANA KWA ALLAH

Kimeandikwa na:
**Muhammad Ali Zanjibari**

# رأيـة الله

تأليف

محمّد علي زنجباري

باللغة السواحلية

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page iii

**© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 - 512 - 84 - 3**

Kimeandikwa na:
**Muhammad Ali Zanjibari**

Kupangwa katika Kompyuta na:
**Hajat Pili Rajab.**

Toleo la kwanza: April, 2011
**Nakala:1000**

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.alitrah.org
Katika mtandao: www.alitrah.info

# YALIYOMO

Utangulizi....................................................................................2

Dibaji...........................................................................................7

Utanabahisho..............................................................................9

Jicho halimwoni Allah............................................................10

Tegemeo la wenye kudai kuonekana kwa Allah......................18

Kumtakasa Mwenyezi Mungu.................................................32

Chimbuko la itikadi hizi..........................................................43

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page v

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA MCHAPISHAJI

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake, hivyo, Mwenyezi Mungu akasema: *"Leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema Yangu na nimewapendeleeni Uislamu uwe dini yenu." (5:3)*

Isipokuwa kuna masuala madogomadogo ambayo wanazuoni wa sheria wamehitilafiana kwa sababu ya kutofautiana kwao kuhusu riwaya ambazo zimenasibishwa kwa Mtume. Jambo ambalo limesababisha kutofautiana kuhusu masuala madogomadogo ya sheria na ya kiimani.

Je, Mungu ataonekana? Hili ni suala ambalo wamehitalifiana wanavyuoni wa Shia na Sunni. Kwa ujumla, wanavyuoni wote wa Shia wanakubaliana kwamba Mungu hawezi kuonekana si hapa ulimwenguni wala kesho Akhera. Ili kuliweka wazi suala hili, Sheikh wetu, Muhammad Ali Zanjibari, amelifanyia utafiti wa kina suala hili na kuweka wazi kwamba Mungu hataonekana kwa kutoa ushahidi kutoka kwenye Qur'ani na hadithi za Mtukufu Mtume S.a.w.w

Katika kuwasilisha hoja zake, mwanachuoni huyu alitumia rejea za vitabu vingi mashuhuri vikiwemo vya Kisunni. Rejea na vitabu hivyo vimeorodheshwa katika tanbihi chini ya kurasa ndani ya kitabu hiki ili msomaji aweze kuvirejelea.

Ni muhimu kufikia kila aina ya maoni katika kujaribu kuamua ukweli. Uislamu kimsingi uko dhidi ya kufuata kibubusa. Ni muhimu mtu kuelewa hoja za wale ambao hakubaliani nao. Inawezekana kusemwa kwamba wale ambao hawaelewi kabisa mtazamo wa maoni tofauti, hawaelewi kwa ukamilifu (mtazamo) wa kwao wenyewe.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Muhammad Ali Zanjibari kwa kuandika kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**
**S. L. P. 19701**
**Dar-es-Salaam, Tanzania.**

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 1



Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 2



# UTANGULIZI

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu, Muumba wa dunia hii, Rehma na amani zimshukie Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pamoja na ahli zake wote. Qur'ani tukufu inawataka wanaadamu kutafakari na kuzingatia hasa katika vile vilivyoumbwa na Mungu ili waweze kuzielewa siri za maumbile. Mwanadamu anatakiwa aifikirie hali yake, matendo yake na nafsi yake. Kuzingatia matukio ya kihistoria kunapelekea kuweza kuelewa asili ya mambo yalivyo. Hivyo, Uislamu unaiona tauhidi ambayo, ndiyo kielelezo hasa cha upweke wa Mungu, kama jambo la msingi ambalo ni wajibu kulitafakari na kulizingatia.

Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillah (a.s.), kuwa siku moja Imam Ali (a.s.) alipokuwa anahutubu juu ya Mimbari ya msikiti wa mji wa Al-Kufa, huko Iraq, mtu mmoja aliyeitwa Daalabu alisimama na kumuuliza: "Ewe Amirul-Mu'minin, umewahi kumwona Mola wako? Imam akasema: "Ole wako ewe Daalab, mimi siwezi kumuabudu Mungu nisiyemuona." Daalab akasema: Ewe Imam, umemuonaje? Imam akajibu kwa kumwambia: "Ewe Daalab, elewa kuwa macho hayawezi kumuona kwa kumtazama bali nyoyo ndizo zinazomuona kutokana na ukweli wa imani**…**

﴿لَّا تُدۡرِكُهُ ٱلۡأَبۡصَٰرُ وَهُوَ يُدۡرِكُ ٱلۡأَبۡصَٰرَۖ وَهُوَ ٱللَّطِيفُ ٱلۡخَبِيرُ ١٠٣﴾

**"Macho hayamfikii kumuona bali Yeye anayafikia macho naye ni mwenye kujua yaliyojificha na yaliyo dhahiri" Sura Aan'am, aya ya 103** [i]

---

i*"A Shiite Anthology"*, Allamah Sayyid Muhammad Husayn Tabatabaiy, uk. wa 38-39.

## Kuonekana kwa Allah

Upweke wa Mwenyezi Mungu ni haki isiyo shaka na ipo haja ya kueleza mipaka ya asili ya kumpwekesha Allah (*tawhid*) na ile mipaka inayopelekea ushirikina (*shirk*), jambo hili linalohitajia vielelezo na mazingatio makubwa kwa vile ndio hasa mzizi mkuu wa dini yenyewe. Qur'ani imewasisitiza watu kutafakari kwenye maumbile na maajabu yake ili wapate kumuelewa Muumba hasa wa maumbile hayo. Mara nyingine Qur'ani huashiria hayo kwa kusema:

**"Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na katika kupishana kwa usiku na mchana, na katika vyombo vipitavyo baharini kubeba yale yenye faida kwa watu, na katika maji aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu kutoka mawinguni ambayo kwayo ameihuisha ardhi baada ya kuchakaa, kisha akaeneza humo aina zote za wanyama, na katika mabadiliko ya pepo na mawingu yaliyoamriwa kupita baina ya mbingu na ardhi; bila shaka katika haya zimo ishara kwa wenye akili."[1]**

Mwislamu anatakiwa azingatie haya yote ili aelewe uwezo, sifa, na hatimaye dhati[2] ya Mola Wake. Inasikitisha kuona kuwa Waislamu sasa wameiacha falsafa hii ya kutafakari kwa kutumia vipaji na akili zao.[3] Matokeo ya jambo hili ni kwamba kumepatikana watu

1 - Surat Al- Baqarah, aya ya 164.

2 Dhati ya Allah haieleweki. Kwa hivyo, jua ndugu msomaji kwamba makusudio yangu juu ya kuijua dhati ya Allah, ni vile kutokuijua kwani, kama ilivyosemwa, kutokumdiriki Allah ndio kumdiriki kwenyewe.

3 Sikusudii kusema kwamba tuitangulize akili kuliko Sharia, bali nakusudia kusema kwamba tutumie akili katika kuisoma Sharia, kwani Sharia haigongani na akili. Naam! Yako mambo ambayo akili ya binaadamu haina uwezo wa kuyafahamu. Mambo haya ni baadhi ya mambo ya Sharia: si mambo ya kiakili. Mfano wa hayo ni kama vile ni kwa sababu gani tusali rakaa mbili alfajiri na nne adhuhuri; kwa nini tuzunguke al-Ka'aba n.k. Lakini, tena, elewa kwamba kuna tofauti baina ya mambo ambayo yanagongana na akili na mambo ambayo akili haina uwezo wa kuyafahamu. Mambo hayo tulioyataja hapo si kwamba yanagongana na akili bali ni mambo ambayo akili ya kiumbe haiwezi kuyafahamu. Ama mambo yanayohusiana na sifa za Allah ni mambo yanayofahamika kiakili. Huoni kwamba akili timamu haihitaji andiko ili kujua kuwa Allah ndiye Muumba, Muweza, Mwenye elimu n.k.

wanaokataa kabisa kutumia akili zao katika Uislamu. Kwa ajili ya hayo kukapatikana Waislamu wanaoitwa *"ahlu-dhwahiri,"* ambao ni wale waliozichukua hadithi, aya na ibara nyingine kama zilivyo katika maana yake ya juu juu au ya dhahiri. Kuna wengine huitwa "*ahlul-hadith"*. Wengine wakajiita *"assalafiyyah."* Bali hawa walikataa hata kuzifanyia taawili baadhi ya aya za Qur'ani ili kupata maana sahihi inayokubaliana na fikra ama akili zilizoumbwa na Mungu. Hayo ndio maradhi yaliyotukumba, Qur'ani inasema kinaga ubaga kuwa;

﴿ إِنَّآ أَنزَلۡنَٰهُ قُرۡءَٰنًا عَرَبِيّٗا لَّعَلَّكُمۡ تَعۡقِلُونَ ۝٢ ﴾

**"Hakika sisi tumeiteremsha Qur'an kwa lugha ya Kiarabu ili mpate kuifahamu." Surat Yusuf aya ya 2.**

Iwapo Qur'ani imeshuka kwa lugha ya Kiarabu, ni lazima fani na fasihi ya lugha hii imetumika katika Qur'ani; na iwapo haya ni kweli, kwa nini tukatae kuwa katika Qur'ani mna majazi, istiara, na fani nyingine za balagha? Kwa kuwa Kiarabu hakiachani na fani hizi, kwa nini sisi tuzikatae fani hizi tunapofasiri Qur'ani? Suala la kuonekana ama kutoonekana kwa Mwenyezi Mungu huko Akhera limezuka kutokana na matatizo mawili:

Moja ni kutokuzichuja riwaya zilizosimuliwa juu ya maudhui hii, kwa kuzitazama *sanad* zake na *matini* zake ambapo Qur-ani ilitakiwa iwe ndio kipimo cha mwanzo cha kuzipima riwaya hizo.

Pili ni tatizo hili tulilolitaja hapa la kutokwenda kwa mujibu wa fani za lugha ya Kiarabu.

Kuzifasiri aya za Qur'ani bila ya kujali taratibu za asili za lugha ya Kiarabu ni kuipotosha Qur'ani yenyewe. Katika kitabu hiki suala la kuonekana kwa Mwenyezi Mungu na macho ya wanaadamu huko Akhera limepingwa kutokana na kukosekana kwa ushahidi wa

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 5



Qur'ani na Sunna za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Pia aya zilizotumiwa kama ni ushahidi wa kuthibitisha kuonekana kwa dhati ya Allah zimeelezwa na kufafanuliwa muradi wake na makusudio yake. Kwa kifupi aya zinazodaiwa na baadhi ya Waislamu kuwa zinathibitisha kuonekana kwa Mungu kwa macho huko Akhera unapozipeleka kwenye fani za lugha yenyewe, maana hizi hazitakubalika kwa vile zinapingana na aya nyingine kama utakavyoona hayo wewe mwenyewe.

Kwa kuwa sisi Waislamu makimbilio yetu ni Qur'ani tukufu, mjadala huu tumeuacha na kuukabidhi kwa Qur'ani ili tupate uamuzi sahihi. Ni matumaini yangu kuwa kitabu hiki kitachukuliwa kama ni chimbuko la kubadilishana mawazo tu wala si ushabiki na tusi kwa yeyote.

Nitakuwa mwizi wa fadhila kama nitaacha kumshukuru ndugu yangu Sheikh Juma Mazrui wa Oman aliyetoa mawazo yake mengi kwangu katika kukamilisha Kitabu hiki kwa lengo la kuufikisha ujumbe huu wa Qur'ani Tukufu. Kwa hakika Sheikh Juma Mazrui amechukua bidii kubwa katika kuniongezea dondoo ambazo katika mazingira niliyokuwa nikiishi ilikuwa ni tabu sana kupata dondoo hizo, kuna uchache wa vitabu hapa nilipo, na wakati wa kutafiti kwangu ulikuwa mdogo kutokana na sababu zisizoweza kuzuilika.

Hakika namuomba Allah azidi kumpa Sheikh Juma Mazrui ufanisi na tawfiiq Duniani na Akhera ili aendelee kushirikina na waisilamu wenzake bila ya kujali rangi zao, kabila zao na madhehebu wanayofuata. Hakika sifa hii ya Sheikh Juma inapaswa kuigwa na kupigiwa mfano. Kama kulikuwa na malumbano ya kimadhehebu baina yangu na Sheikh Juma Mazrui miaka iliyopita ilikuwa amma ni kutokana na shetani au kutokana na nafsi zetu ambazo zilikuwa na hadi leo hii hazijakamilika, lakini nachukua nafasi hii kumlaani shetani na kumweka mbele Allah Subhanahu wataala kwa kila jambo, na namuomba Allah

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 6



akijaalie Kitabu hiki kiwe ni sababu ya kuwaunganisha waisilamu wote Duniani, amin.

Kwa hakika Sunni, Salafi, Shia na Ibadhi wote ni Waisilamu wanaohitajiana na inshaallah Kitabu hiki kitakuwa ndio ni moja ya funguo za fikra ya mlingano na kukurubiana na kuondoa tofauti kati ya waisilamu inshaallah. Ukamilifu wote ni wa Allah na kama kukiwa na kasoro yoyote kwenye kitabu hiki, kasoro hiyo inatoka kwangu natanguliza kuomba msamaha kwa kasoro hizo kwa Allah na kwa waisilamu wote. Ahsanteni.

**Ndugu yenu, Muhammad Ali Zanjbari.**

# DIBAJI

Sifa zote njema zinamstahikia Allah, rehma na Amani za allah zimshukie Hashima Al-Habibi Muhammad (S) na Ahli zake Kirama. Katika Uislamu suala la kumuona Mungu ni suala ambalo Waislamu wamelipa nadharia tofauti. Baadhi ya Waislamu huamini kuwa ni muhali kwa Mwenyezi Mungu kuonekana kwa macho na hivyo wakaishia kwa kuamini kwamba Mwenyezi Mungu haonekani duniani wala Akhera. Sehemu nyingine ya Waislamu iliyobakia huamini kuwa Mwenyezi Mungu haonekani duniani tu, bali ataonekana Siku ya Kiyama na waumini kwa macho yao. Wengine wamediriki kusema kuwa hata duniani Allah ameonekana. Na hawa wamegawika makundi tofauti:

Kundi moja linasema kuwa kuonekana kwa Allah hapa duniani ni mahususi kwa Nabii Muhammad. Imamu Al-Nawawi ni mmoja wa wenye rai hii.[4]

Kundi la pili linasema hata Nabii Musa alikuwa akimuona Allah, lakini alikuwa hajui kwamba ndiye Allah, kama alivyodai Al-Alusi[5] na Al-Qadhi Abu Bakr kama alivyonukuu Al-Qadhi ‘Ayyadh kutoka kwake akisema: “Hakika Musa (a.s) alikuwa akimuona Allah”.[6]

4Tazama Fatawa zilizokusanywa katika kitabu kiitwacho *Al-Masailu Al-Manthura* cha Imamu Al Nawawi kilichochapisha Misr mwaka 1352 H. Pia kaashiria kumili katika rai hii – japo hakusema kwa uwazi – katika *Sharhu Sahihi Muslim* alipokuwa akiisherehesha Hadithi na. 287, na Hadithi na. 283. Ama katika fatawa tulizozitaja mwanzo kasema hivyo kwa uwazi.

5 Tazama Al-Alusi *Ruhu Al-Ma’an* Jz. 9, uk 52. Na miongoni mwa wenye rai hii ni Ibn Batta ambaye amedai kuwa Musa (a.s.) alikuwa akimuona Allah juu ya mti! Tazama *Lisanu Al-Mizan* cha Ibn Hajar Jz. 4, uk. 112-113.

6 Al-Qadhi ‘Ayyadh *Al-Shafa* Jz. 1, uk. 155.

Kundi la tatu linadai kuwa hata Waumini pia wamewahi au wanaweza kumuona Allah hapa duniani. Na hawa wanagawika sehemu tatu:

Wanaosema kuwa waumini wamemuona wakiwa macho. Anasema Al-Bajuri "Na wakatofautiana juu ya kauli mbili za Al-Ash'ari kuhusu kutokea kwake (kuonekana kwa Allah) na Mawalii, iliyo na uzito ni kuwa haonekani".[7] Anasema Sheikh Al-Khalili, Mufti wa Oman,: "Na hakuna aliyesema kuwa (kuonekana kwa Allah) kumetokea kwa asiyekuwa Mtume (Muhammad s.a.w.w.) isipokuwa masufi (*extremists*) waliochupa mipaka ".[8]

Wanaosema kuwa Allah anaweza kuonekana usingizini. Miongoni mwa hawa ni Al-Alusi ambaye anadai kuwa yeye kamuona mara tatu.[9]Na bila shaka Ibn Taymiyya naye anamili katika rai hii. Anasema: "Na huenda muumini akamuona Mola Wake usingizini kwa sura tofauti kwa kadiri ya imani yake, akiwa na imani sahihi basi hatomuona ila katika sura nzuri; ikiwa imani yake ni pungufu basi atamuona kama ilivyo imani yake".[10] Lakini pamoja na hayo, Ibn Taymiyya anasema: "Na kuona usingizini ina hukumu tofauti na kuona katika hali ya macho".[11] Kwa hali yoyote ile, ibara hii haibadilishi ukweli kwamba Ibn Taymiyya anaamini kuonekana kwa Allah usingizini, bali anasisitiza tu kwamba kumuona huko kunakuwa na *ta-awili.*

---

7 Al-Bajuri, *Sharhu Al-Jawhara* uk. 118. Na mfano wake ni maelezo ya Muhammad Adib na mwenzake katika sherehe yao ya kitabu hicho hicho, Jz. 2, uk. 700.

8 Al-Khalili, *Al-Haqqu Al-Damigh* uk. 27.

9 Tazama Al-Alusi *Ruhu Al Ma'an* Jz. 9, uk 52. Na miongoni mwa wenye rai hii ni Ibn Batta ambaye amedai kuwa Musa (a.s.) alikuwa akimuona Allah juu ya mti! Tazama *Lisanu Al-Mizan* cha Ibn Hajar Jz. 4, uk. 112-113.

10 Ibn Taymiyya, *Majmu'a Al-Fatawa* Jz. 3, uk. 248.

11 Ibn Taymiyya, *Majmu'a Al-Fatawa* Jz. 3, uk. 248.

Wengine wakasema kwamba duniani, Allah haonekani ila na Mtume (s.a.w.w.), yaani usiku wa miraji. Hii ndio rai mashuhuri kwa Al-Imamu Abu Hasan Al-Ash'ari na baadhi ya wanavyuoni wa madhehebu yake.[12] Rai hii pia imenasibishwa na Al-Hasan Al-Basari.[13]Zote hizo ni rai za Waislamu na nadharia zao juu ya suala la kuonekana kwa Mungu.

Kitabu hiki kimeeleza vya kutosha juu ya suala hili, na kimefafanua kwa kuzijadili kimataifa dalili za kila kundi na hatimaye kutoa ufumbuzi wa suala lenyewe. Ni matumaini yangu kuwa Waislamu wa Madhehebu zote watafaidika na mwangaza huu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu atuwafikishe, tukisikia maneno, tufuate yale yaliyo mema zaidi.

## UTANABAHISHO

Mwandishi wa kitabu hiki hana nia wala lengo la kuwarudi wale wenye itikadi iliyo kinyume na yeye, bali lengo lake hasa ni kuzichemsha fikra za wasomaji na ndugu zake Waislamu kwa kutoa na kuandika rai zake juu ya mas'ala haya ambayo ni muhimu katika lengo la kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kuifuata Qur'ani Tukufu. Ingawa katika kueleza rai zake mwandishi wa Kitabu hiki imebidi kutoa ushahidi mbali mbali na kuzipinga kauli za waisilamu wengine, hii ionekane kama ni zawadi ya kielimu badala ya hali ya mjadala na ushindani wa kimadhehebu, hakika nia ni kuwaweka waisilamu wote kwenye Qur'ani na Sunnah sahihi za Mtukufu Mtume Muhammad (S).

12 Al-Qadhi 'Ayyadh, *Al-Shafa* uk. 154. Muhammad Adib *Jawhara Al-Tawhid* Jz. 2, uk. 704.

13 Marejeo yaliyotangulia.

Ni matumaini yangu kuwa nyote mtafaidika na Kitabu hiki ambacho ingawa ni kidogo kwa kurasa zake lakini hapana shaka kimekusanya kila la maana katika mada hii, hakika ukumbusho huwafaa waumini.

Nawatakia kila la kheri katika kusoma Kitabu hiki, Mola awape tawfiq na uongofu na aziunganishe nyoyo zenu na haki au na kila la kheri analoliona Yeye Subhanahu kwenye Dhati Yake iliyotakasika na Aibu au Kasoro, amin!

**Ahsanteni.**

**Jaffar Muhammed Ali.**

## JICHO HALIMWONI ALLAH

Ni katika mambo yaliyo maarufu katika Uislamu kuwa Mwenyezi Mungu (swt.) anatofautiana na viumbe vyote katika dhati Yake, sifa Zake na hatimaye kwenye vitendo Vyake. Yeye hawezi kufananishwa na kitu chochote, wala hakuna kitu kilichofanana naye, na wala Yeye hawezi kuambiwa kuwa ni kitu ambacho labda kina upana, ama kiwiliwili, na kadhalika. Mwenyezi Mungu aliyetakasika hasifiwi, wala hasifiki, na sifa ya kuwepo mahala fulani, au kutokea wakati fulani. Mahala na nyakati hazina uhusiano na Mwenyezi Mungu kwani Mwenyezi Mungu amekuwepo kabla ya kuumbwa kwa nyakati na sehemu. Mwenyezi Mungu yupo kama ambavyo alitangulia kuwapo bila ya kuwa na pahala, haonekani kwa jicho wala hauliziwi alipo. Kwani kuulizwa yu wapi ni kwa yule au kile ambacho hukaa mahala maalum na kuchukua nafasi, hivyo sifa zote za viumbe ni muhali kupatikana kwa Mwenyezi Mungu.

Kutokana na hayo, dhati ya Mwenyezi Mungu haionekani kwa macho wala kwa hisia za binadamu zenye kuambatana na hisia za kimwili na ulimwengu wa dhahiri au kwa kumfikiri. Waislamu wametofautiana

katika suala la kuonekana kwa Mungu. Baadhi ya Waislamu wanaamini kuwa Mwenyezi Mungu haonekani duniani tu, bali ataonekana huko Akhera (Siku ya Kiyama). Waislamu wengine huamini kuwa ni muhali kwa Mungu kuonekana ni sawa hayo duniani au Akhera. Na lililo la ukweli na ambalo halina wasiwasi juu ya suala hili ni kuamini kuwa Mwenyezi Mungu haonekani kwa macho duniani na hataonekana na macho huko Akhera. Haya ya kutoonekana duniani na Akhera ameyaeleza Mwenyezi Mungu (swt.) mwenyewe pale alipojieleza alivyo kama ilivyo katika aya ifuatayo

**"Macho hayamfikii kumuona bali yeye anayafikia macho (na kuwaona wenye macho), naye ni mwenye kujua yaliyofichikana na yaliyo dhahiri".**[14]

Katika suala hili, wanaotaka kuthibitisha kuonekana kwa Mungu huko Akhera wanafasiri tamko la - *al-idrak* – kwa maana ya 'kuzunguka! Na hayo ni makosa makubwa kwa sababu neno hilo halina maana hiyo, bali katika vitabu vya lugha neno hilo linapotumika bila ya kufungamanishwa na kitu, basi huwa lina maana ya *"kufikia"*.[15]Kamusi za kiarabu na Waarabu wenyewe hulifasiri neno hilo hivyo. Ama linapofungamanishwa na kiungo fulani au kitu fulani, basi elewa kwamba *idrak* ya kila kiungo au kila kitu na kwa vile kilivyo. *Idrak* ya mkono ni kushika. Ukisema *Al-Yadu laa tudrikuhu* (mkono haumdirki), maana yake mkono haumfiki ukamshika. *Idrak* ya sikio ni kusikia. Ukisema *Al-Udhnu laa tudrikuhu* (sikio halimdiriki), maana ni sikio halifikii yaani halimsikii. Halikadhalika ukisema *Al-Basaru la yudrikuhu* (jicho halimdiriki) maana ni jicho halimfiki yaani halimuoni. Na kwa hivyo, Aya isemayo: "Jicho halimdiriki" maana ni "Jicho halimfiki" na kufikiwa na

14 **Surat-Al-an'am Aya ya 103**.

15 - Tazama

jicho ni kuonekana. Kwa hivyo, maana ni "Jicho halimuooni": si jicho halimzunguki. Pia anasema mwenye kamusi liitwalo *Taju Al-Arus:* "Al-Darak (yaani Al-Idrak) maana yake ni kufikia".[16] Anasema Al-Jawhari: "Al-Idrak maana yake ni kufikia".[17] Anasema Ibn Mandhur: "Al-Darak (yaani Al-Idrak) maana yake ni kufikia" na katika Qur'ani (Aya inasema): حَتى إذا ادّارَكوا فيهَ *(Hatta idha ddarakuu fiha)* "Hata watapofikiana humo (kwenye moto)".[18] Yaani kila kundi moja likalifikia kundi jengine: wala si makusudio ya Aya hii kwamba kila kundi moja litalizunguka jengine.

Kwa maana hii, elewa kwamba Waarabu wanaposema: "*Adraktuhu bi-Aynay"* (nimemdiriki kwa macho yangu), basi wanakusudia kusema kuwa, "Nimemwona kwa macho yangu". Mfano kama huu umekuja katika kitabu cha lugha ya Kiarabu ambacho Waarabu wenyewe wanakitegemea. Basi itasemwaje kuwa, *"Al-Idrak"* inamaanisha "kuzunguka?" Na Waarabu wanaposema, *'Adraktu hayata fulan'*, huwa wanakusudia kusema kuwa, "nimemwahi fulani" yaani, "nimezaliwa kabla hajafa" na wala usemi huu hauna maana kuwa aliyesema hivyo ni lazima awe ameuzunguka uhai wote wa mtu huyo tangu alipozaliwa hadi kufa kwake. Halikadhalika inaposemwa, *Adrakahu Ssahamu"*, humaanishwa kuwa, "mkuki umempata", iwapo atalengwa nao na ukamchoma. Kwa upande mwingine, tunaona kuwa Bibi Aisha (r.a.) anakanusha maneno ya watu ambao, mbali na kuwa wanaamini kuwa Mungu ataonekana huko Akhera (Kiyama), wamediriki hata kudai kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwona Mola Wake katika usiku wa Miiraj! Jee, dai hili ni kweli? Lakini kinyume chake tunaona kuwa Imam Al-Bukhari na Imam Muslim wamesema kuwa (Bibi Aisha (r.a.) amesema, "Asemaye moja

16 *Taju Al-'Arus* Jz. 7, uk. 126.
17 *Al-Jawhari Al-Sihah* Jz. 4, uk. 1582.
18 Ibn Mandhur, *Lisanu Al-'Arab* Jz. 3, 1363.

kati ya matatu atakuwa amezidisha uzushi kumzulia Mola Wake."[19] Hadithi hii ambayo ameirawi Masrouq kutoka kwa Bibi Aisha (r.a.) inasema kuwa:

"Asemaye kuwa Muhammad amemwona Mola Wake, basi amemzulia Mwenyezi Mungu Uzushi Mkubwa," Masrouq akasema: 'Ewe mama, nipe nafasi wala usiniharakishe. Je Mwenyezi Mungu si amesema kuwa, "Na Mtume akamwona mara nyingine"[20] na (huoni pia kuwa) Mwenyezi Mungu amesema, "na hakika yeye alimwona kwenye upeo wa Macho ulio safi wa Mbinguni."[21]

Baada ya Masrouq (r.a.) kuuliza hayo, Bibi Aisha (r.a.) akajibu kwa kusema:

"Mimi ni mtu wa mwanzo katika Umma huu kumwuliza Mtume (s.a.w.w.) habari hiyo. Akasema tena, muradi wa hayo ni Jibriil na si Mungu, na huyo Jibriil sikumwona katika Sura yake aliyopewa na Mungu, isipokuwa mara mbili tu." Kisha Bibi Aisha akasema, je, hujasikia kuwa Mwenyezi Mungu (swt.) amesema:

لا تُدْرِكُهُ الأَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الأَبْصَارَ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ

**"Macho hayamfikii kumuona bali Yeye anayafikia macho naye ni mwenye kujua yaliyojificha na yaliyo dhahiri" Sura Aan'am, aya ya [22]**

Yote hayo yanathibitisha kuwa maana ya neno *idrak* linapofuatana na neno *absaar* humaanisha kuona kwa jicho. Vyenginevyo Bibi Aisha (r.a.) asingelikanusha kuonekana kwa Mungu kisha akaifanya Aya hiyo kuwa ni dalili na ushahidi wa kutoonekana huko. Ni wazi kwam-

19 **(i)** *Musnad Imam al-Rabi'i***,** Juz.3, Uk. 226-227, Chapa ya Maktaba ya Istiqamah. (ii) *Sahiih Al- Bukhari***,** Kitab at-tawhid; Hadithi namba: 6,904**.**

20 **Surat An Najmu aya ya 13.**

**21 Surat At-Takwiir aya ya 23.**

**22 Al-An-am aya ya 103.**

ba yeye alijua kuwa lugha iliyotumika humo *"laa tudrik"* imemaanisha kutowezekana kuonekana. Hivyo Aya hii tukufu inakanusha dai kwamba *Idrak* maana yake ni kukizunguka kitu. Kwani – kama tulivyotangulia kusema kwamba – unaposema kuwa mkono umediriki maana yake ni kushika, na huko kudiriki kwa jicho ni *kuona*, hivyo inaposemwa *"La Tudriku Hul absaar,"* maana yake ni kuwa jicho au macho hayawezi kumwona. Sikio nalo kwa mujibu wa lugha ya kiarabu linadiriki na kudiriki kwa sikio ni kusikia yazungumzwayo. Na kudiriki kwa silaha (*Adrakahu Silah)* huwa ni kumpiga silaha aliyotungwa nayo na hivyo ndiyo Kiarabu kinavyokubali, na ieleweke wazi kuwa, na hii Qur'ani imeshuka kwa lugha hii hii tunayoieleza fasaha yake.

Wapo waliodai kuwa aya hii imekusudiwa kutoonekana kwa Mungu hapa duniani tu, na sio Akhera. Itapendeza kwa watu hao kuelewa kuwa, sifa za Mwenyezi Mungu hazibadiliki, hivyo wanapodai kuwa Mungu ataonekana huko Akhera, ndio kusema sifa hii ya kutoonekana kwa macho huko Akhera itamtoka yeye Subhanahu Wataala? Itakumbukwa kuwa Mwenyezi Mungu amejisifu kwa sifa nyingi ndani ya Qur'ani pamoja na kujikanushia mambo mengi ambayo hayalingani na Uungu Wake. Katika kujikanushia usingizi, Mwenyezi Mungu ameikataa sifa hii kwa kusema: **"Kusinzia hakumshiki wala kulala."**[23] Katika kueleza kuwa Yeye Allah hafanyi dhulma, amesema: **"Na Mola wako hamdhulumu ye yote".**[24] Katika suala la kuzaa na kuzaliwa Mwenyezi Mungu amejikanushia hayo; hivyo Yeye hapatikani kwa kuzaliwa na wala hazai. Qur'ani imelitatua suala hili kwa ibara zilizo wazi kama ifuatavyo: **"Hakuzaa wala hakuzaliwa wala hana anayefanana naye."**[25]

23 **Surat Al-Baqarah aya ya 25.**
**24 Surat Al-Kahf aya ya 49.**
**25 Surat Al-Ikhlas aya ya 3-4**.

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 15



Kama tungeifuata hoja ya wanaosema kuwa aya ya 103 ya **Surat Anam** inakana tu kuonekana kwa Mungu na macho ya mwanadamu hapa duniani, ingetubidi pia tuamini kuwa yale yote aliyojikatalia Mwenyezi Mungu katika Qur'ani, Muradi wake ni hapa Duniani tu basi huko Akhera atakuwa na sifa za kuzaa na kuzaliwa au itawezekana pia kudai kuwa Mola atadhulumu huko Akhera au atakuwa na anayefanana naye. Ikiwa mtu atadai kwamba hayo hayawezekani kwa sababu ni mambo yanayoonesha upungufu, na ni kinyume kabisa na sifa za Allah ambaye kakamilika. Basi nasi tutamfahamisha mtu huyo kwamba na kuonekana pia ni sifa inayokwenda kinyume na utukufu wa Allah. Akiuliza nini ushahidi wako? Nitamsomea Hadithi aliyoipokea Imam Muslim isemayo: **"….Na hakuna kitachozuia watu (wa peponi) kumtazama Allah (kumuona) isipokuwa vazi lake la kibri."[26]** Ni wazi kwa mujibu wa riwaya hii, kwamba kibri na utukufu wa Allah ndio uliomfanya asionekane. Suala la kujiuliza ni: je inajuzu kwa Muislamu kusema kwamba iko siku au wakati Allah ataondoa hili vazi la kibri na utukufu ili aweze kuonekana? Kwa lugha nyengine je iko siku Allah atakuwa bila ya kibri na utukufu na badala yake awe dhalili ili tuweze kumuona? Kwa kweli riwaya hii moja ilitosha kutoa jawabu na ufumbuzi wa suala zima hili la kumuona Mungu.

Kwa hivyo, utaona kwamba haifai hata kidogo kusema kuwa aliyojikatalia Mwenyezi Mungu katika nafsi yake amejikatalia kwa hapa duniani tu bila ya Akhera. Wala haitafaa kusema kuwa huko Akhera atakuwa na sifa za kuzaa na kuzaliwa au kuwa na mke, *hashalillah.* Qur'ani inasema:

﴿ إِنَّ عَلَيْنَا لَلْهُدَىٰ ﴿١٢﴾ وَإِنَّ لَنَا لَلْآخِرَةَ وَالْأُولَىٰ ﴿١٣﴾ ﴾

**"Hakika muongozo ni juu yetu sisi. Na ni yetu akhera na dunia. Suratul Layl, aya ya 12:13.**

[26] Kapokea Al-Imamu Al-Bukhari na Al-Imamu Muslim katika Jz. 2 Hadithi na. 296, na wote wameipokea kutoka kwa Abu Musa Al-Ash'ari.

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 16



Na katika Aya nyengine tunasoma:

﴿ فَلِلَّهِ ٱلْآخِرَةُ وَٱلْأُولَىٰ ﴿٢٥﴾ ﴾

**"Basi akhera na dunia ni ya Allah." Sutatul Najm, aya ya 25.**

Maana ya hayo ni kwamba ni juu yake Yeye Mola Uongofu wa watu Kiitikadi na Kielimu na kwamba Dunia na Akhera ni milki ya Mola na kwake Dunia na Akhera ni sawa, kwa maana ya kwamba hakuna tofauti baina ya dunia na Akhera mbele ya Mwenyezi Mungu – zote hazimuathiri kitu, alivyo sasa ndivyo alivyokuwa na ndivyo atavyokuwa. Tunasoma pia katika Qur'ani tukufu kuwa, *"Wala tajidu lissunnatina tahwiyla."* **Surat Israa, aya ya 77.** Yaani; "Wala hutaona mabadiliko kwenye nyendo zake Allah". Basi tunafahamu kuwa, Mola na sifa zake vyote havibadiliki, hivyo iwapo tamko **"Lan tarani",** (hutaniona) humaanisha kuwa hayo ni hapa duniani tu kama wanavyodai wenye kuitakidi kuonekana kwa Allah, madai hayo yatakuwa kinyume na dhati ya Allah kama ilivyo kwenye hiyo aya ya 77 ya **Surat al-Israa** na nyinginezo.

Haya yote yanatupa dalili kuwa Mwenyezi Mungu aliposema, **"Macho ya watu hayamfikii kumuona",** alikuwa anakusudia katika kauli yake hiyo kule kutowezekana kwa macho kumwona yeye duniani na Akhera. Kuna baadhi ya waliodiriki kudai kuwa muradi wa Mwenyezi Mungu kujisifu kwa kujikanushia baadhi ya sifa ni kuthibitisha sifa hizo juu yake na wakasema kuwa kusudio la Mwenyezi Mungu aliposema: **"Haumchukui usingizi wala kulala",** kuna maana ya kujisifu kwa uhai wa maisha. Wakadai pia kuwa kusudio la Mola kujikanushia kuwa na mke na kuzaa ni kuthibitisha jambo jingine! Ama kuonekana kwa Mungu ni sifa aliyojisifu nayo. Na hayo ndio madai ya Ibnul Qayyim aliyefuata maneno ya Sheikh wake Ibnu Taymiyyah[27] ambaye ndiye hasa chimbuko la fitna katika Uislamu.

27 Tazama Ibn Al-Qayyim *Hadi Al-Ar-wah* uk. 215, chapa ya mwanzo1996 Maktaba Al-Iman.

Tunawajibu kuwaeleza kuwa Mwenyezi Mungu amejikanushia Nafsi Yake mambo yote yasiyolingana na alivyo au utukufu Wake na Enzi Yake. Na laiti tungelisema kuwa inafaa kuthibitisha aliyoyakanusha, basi, tungelifanya makosa makubwa, na huko kuyapotoa maneno ya Allah, kwa maneno na methali alizozitaja Ibnul-Qayyim italazimika kwetu tuukimbie ukweli na uhakika na hatimaye tuingie katika mawazo ambayo ni dhana. Na tangu lini dhana hupewa uzito katika kuthibitisha jambo? Mwenyezi Mungu anasema: Yaani, **(hakika ya dhana haiitoshelezi haki kitu cho chote!)**[28]

Zaidi ya haya, kuna hadithi za kweli zitokanazo na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zinazokataa kuonekana kwa Mwenyezi Mungu (swt.). Baadhi ya hadithi hizo ni kama ile iliyokuja katika ***Sahih Muslim*** kwa Sanad ya Abu Dharr pale alipomwuliza Mtume (s.a.w.w.) kwa kusema “Jee, umemwona Mola Wako usiku wa Miiraj?” Mtume akajibu kwa kusema. “Nuru basi vipi nitaiona?” Maneno haya yanadhihirisha kwa uwazi kukanusha kwa Mtukufu Mtume kuwa kamwona Mola Wake. Na ndio maana tukasema kuwa sifa za Mungu alizokuwa nazo tangu na tangu hazibadiliki maana yeye *Subhanahu Wataala* si mwenye kubadilika. Na kwa hiyo haiwezekani kwa Mungu kuwa na sifa fulani na kwa muda fulani tu, bali sifa zake ni za tangu na tangu na milele. Kuna dalili za kiakili zinazoweza kusaidia kukanusha kuonekana kwa Mwenyezi Mungu. Miongoni mwa hizo ni kuwa; kuona kunahitaji mambo ya lazima, nayo ni kuwepo kwa mahali; na mahali hapo pawe na nafasi inayomkabili mtazamaji bila ya sehemu hiyo kukaribiana sana, wala isiwe mbali sana na jicho. Kisha hicho kinachotazamwa kiwe ni kiwiliwili ama umbo lenye kuchukua nafasi, kisiwe kitu kama hewa ama sauti. Yote hayo yanahitajika ili kitu kionekane, hayo yote ni kinyume cha dhati ya Mwenyezi Mungu na utukufu Wake.

28 **Surat Yunus aya ya 36.**

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 18



# TEGEMEO LA WENYE KUDAI KUONEKANA KWA ALLAH

Waislamu wanaodai kuwa Mwenyezi Mungu ataonekana Siku ya Kiyama wanaitegemea aya isemayo:

﴿ وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ ﴿٢٢﴾ إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ ﴿٢٣﴾ ﴾

(a). **"Nyuso nyingine siku hiyo zitang'ara kweli kweli huku zikimtazama Mola Wao" Surat Al-Qiyama aya ya 22-23).**

**Tanbihi:** Tafsiri sahihi ya aya hiyo ni:
(b) "Nyuso nyingine siku hiyo zitang'ara kweli kweli "zikisubiri kupata neema za Mola Wao."

Tafsiri iliyoko kwenye kifungu (a) ndio tafsiri ya wengi kati ya *Ahlul Sunnah* na wenzao wanaojuzisha kuonekana kwa Allah Siku ya Kiyama. Hivyo wao wamelifasiri neno **NADHIRA** kwa maana ya 'kutazama' na 'kuona' na ndio maana unakuta kuwa wengi wao huamini kuwa aya hii ni katika aya iliyothibitisha kuonekana kwa Mwenyezi Mungu hapo Siku ya Kiyama. Tafsiri ya aya hiyo iliyoko katika kifungu (b) ni tafsiri inayokubaliwa na Waislamu wa madhehebu ya ***"Ahlul-bayt"*** (Shia) na madhehebu ya Kiibadhi na Mu'tazillah na wenzao wasiokubali kuonekana kwa Allah kwa macho Siku ya Kiyama. Kutokana na aya hii wao wakalifasiri tamko la *nadhira* kuwa ni kusubiri neema ama rehema za Mola. Inshaallah tutaeleza juu ya aya hii kwa kirefu kama ilivyo hapa chini.

Tunasema kuwa ndugu zetu hawa wanaojuzisha kuonekana kwa Allah kwa macho ya utosini Siku ya Kiyama wameifasiri aya hiyo na kusema kuwa, 'nyuso zinamtazama Mola Wao,' lakini maana ya neno

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 19



***NADHIRA*** hapa sio kutazama bali ni kusubiri yaani watakuwa wakisubiri au kutazamia rehema za Mola Wao ili waingie peponi. Dalili ya kuwa hao watu wema watakuwa wakisubiri kupata rehema za Mola Wao na sio kwamba watakuwa wakimtazama Mola Wao ni kuwepo kwa huu mkabala (*opposite*) wa kibalagha. Ni vyema kujua kwamba Qur'ani imeteremka kwa lugha ya Kiarabu iliyo fasaha, na wala mfumo wake haukwenda kinyume na mfumo wa Kiarabu fasaha. Na wanavyuoni wa Balagha ya Kiarabu wanabainisha katika vitabu vyao kwamba sentensi moja inapokuwa katika *muqabala* (opposite) na nyingine, basi moja huwa ni kinyume na ya pili. Sasa ukitazama Aya hiyo "**Nyuso nyingine siku hiyo zitang'ara kweli kweli huku zikimtazama Mola Wao",** kama wanavyoifasiri wao. Au **"Nyuso nyingine siku hiyo zitang'ara kweli kweli "zikisubiri kupata neema za Mola Wao",** kama tafsiri sahihi ilivyo, basi utaona kwamba kwa upande mwingine aya zinasema kuwa kutakuwa na kundi la wabaya ambao Qur'ani inawaeleza kwa kusema: **"Na nyuso zingine siku hiyo zitakunjamana".**[29] Aya hii inakabiliwa na aya **"Kuna nyuso siku hio zitang'ara":** hizi zitang'ara kwa furaha na nuru; na – kinyume chake – nyuso za pili zitakunjana kwa huzuni na kama kwamba zimetandwa na kiza. Hapa utaona kuwa *muqabala (opposite)* baina ya nyuso hizo umepatikana.

Kisha Qur'ani inaendelea kuwaeleza watu wabaya katika aya hiyo ya 24, ya **Surat Al-Qiyama** kwa kusema: **"Zitajua ya kuwa zitafikiwa na msiba uvunjao uti wa mgongo."**[30] Yaani nyuso hizo za watu wabaya zitakuwa zinatazamia hali hio. Ukiyatazama maneno ya aya hii, utayakuta yakabiliana (ni kinyume) na maneno ya aya ya 22-23 yanayozungumzia nyuso za watu wema kwamba **"Nyuso nyingine siku hiyo zitang'ara kweli kweli "zikisubiri kupata neema za Mola Wao".** Na natija ni kuwa:

**[39]Surat Al-Qiyama aya ya 24.**

**[30] Surat Al-Qiyama Aya ya 25.**

Nyuso za watu wema zitasubiri (zitatazamia kupata) rehema.
Nyuso za watu wabaya zitatazamia adhabu.

Na hapa utaona kwamba *mkabala* (kinyume au *opposite*) wa balagha ya Kiarabu umepatikana.

Ama ingelikuwa ni sahihi kusema kuwa nyuso zitamtazama Mola Wao (ili zimuone), ingebidi na zile aya za upande wa pili ziseme kuwa, "nyuso nyingine siku hiyo zitakunjamana na hazitaweza kumwona Mola Wao." Au kungesemwa maneno yenye maana kama hii. Pia elewa kwamba kudai kuwa Aya ina maana ya kumuona Allah, basi ni kuubomoa msingi huu wa lugha kwa nguvu za kiitikadi. Inavyotakiwa kanuni za tafsiri ziwe ndio msingi wa kuzaa itikadi: sio kuwa itikadi iwe ndio msingi wa kuzaa tafsiri. Lau tutaifasiri Aya hio kuwa maana yake ni kumuona Allah, basi maana itakuwa:

Nyuso siku hio zitang'ara: zikimuona Mola Wao.

Na Nyuso (nyengine) siku hio zitakunjana: sikisubiri adhabu.

Uko wapi *mkabala* (*opposite*) katika tafsiri hii? Je kuona kinyume chake ni kutazamia kuja kwa kitu au kukijua kitu? Ni wazi kwamba hapa tafsiri yao hii ni kinyume na mfumo wa lugha ya Kiarabu. Na kwa hivyo, ni tafsiri batili. Ama dai lao kuwa laiti neno **"NADHIRA"** lingekuwa na maana ya **KUSUBIRI** lisingefuatana na "harfu-jar" **(ILA)** na kwa kuwa limefuatana na **ILA** itamaanisha **KUTAZAMA**, tunasema kuwa dai hilo si sahihi**.** Nasi tunajibu hoja hio kwa kusema kuwa, maneno ya Waarabu yanakubali hivyo na mashairi ya Kiarabu ya asili yamejaa mifano na ibara zinazosema, "*Nadhara ila,*" kwa maana ya kusubiri. Lakini sisi natutosheke na mifano ya Qur'ani, Mwenyezi Mungu amesema:

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 21



﴿ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَشۡتَرُونَ بِعَهۡدِ ٱللَّهِ وَأَيۡمَٰنِهِمۡ ثَمَنٗا قَلِيلًا أُوْلَٰٓئِكَ لَا خَلَٰقَ لَهُمۡ فِي ٱلۡأٓخِرَةِ
وَلَا يُكَلِّمُهُمُ ٱللَّهُ وَلَا يَنظُرُ إِلَيۡهِمۡ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ ﴿٧٧﴾ ﴾

**"Hakika ya wale wanaouza ahadi ya Mwenyezi Mungu na viapo vyao kwa ajili ya thamani ndogo ya ulimwengu, hao hawatakuwa na sehemu ya kheri katika Akhera, wala Mwenyezi Mungu hatasema nao wala hatawatazama siku hiyo ya Kiyama". Surat Al-Imran Aya ya 77**.

Hapa katika Aya hii neno **"NADHIRA"** limefuatana na "harfu-jar" **(ILA);** suala ni: je, maana ya maneno, "wala hatawatazama siku hiyo ya Kiyama" – ambalo Kiarabu chake ni وَلا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيامَة ni kusema, kuwa Mola atakuwa hawaoni? Na kwamba atawaona baadhi ya viumbe Wake tu? Bali hayo si kweli na Mungu ametakasika na hayo na kusudio la maneno hayo ni kuwa Mwenyezi Mungu siku hiyo hatawapa rehema Zake. Kwa maana hii twaweza kufahamu kuwa kumtazama Mola mja Wake ni kumpa rehema na msaada bali mja kumtazama Mola Wake ni mja kusubiri akingoja kurehemiwa na kupewa neema na Mola Wake. Jambo la pili la kufahamu hapa ni kuwa uhakika wa kuona huwa daima ni kwa macho: na sio kwa uso; na hili laeleweka wazi na kwa wote. Hebu sasa natujiulize, ni kwa nini zimetumika nyuso katika aya hii: pasi na kutumika neno macho? Jawabu ni kwamba, kutumika kwa nyuso badala ya macho ni jambo la **MAJAZI** tu, wala si la hakika na vipengele kama hivi ni maarufu kwenye balagha ya Lugha ya Kiarabu.

Unaweza kujiuliza suala jingine ukipenda, nalo ni, kwa nini zikatajwa nyuso tu badala ya viungo vingine vya mwili? Na hali tunajua kuwa kutazama kitu tukipendacho huanza kufurahia moyo kwanza kabla haujafurahi uso na baadaye kuenea furaha na hivyo kiwiliwili chote. Yote haya yanathibitisha kuwa *'Nadhara'* katika Aya hii ina maana ya

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 22



*"Kusubiri"* na wala haina maana ya *'kuona'* asilani! Qur'ani pia imelitumia neno hili "nadhara" au "nadhira" kwa maana ya "kungo-ja" au "kusubiri", katika sehemu nyingi kama ilivyo kwenye aya:

وَإِنْ كَانَ ذُو عُسْرَةٍ فَنَظِرَةٌ إِلَى مَيْسَرَةٍ

*"Wain kana dhu-usratin **fanadhiratun** ila maysarah".*
"Na iwapo mko kwenye dhiki, basi ngojeni hadi *mtapofarijika*."[31]

Halikadhalika Allah aliposimulia habari za Iblis, utaona kwamba amelitumia tamko hilo hilo la "nadhira" kwa maana ya kungoja" na "kusubiri", Qur'ani Tukufu ikiashiria haya inasema:

﴿ قَالَ رَبِّ فَأَنظِرْنِي إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ ۝٣٦ قَالَ فَإِنَّكَ مِنَ الْمُنظَرِينَ ۝٣٧ ﴾

*"Qala rabbi **fandhirni** ila yawmi yub'athuun, Qala innaka minal **mundhariin**."*

**"Akasema Mola wangu, nipe muda hadi siku ya Kiyama. Mungu akasema, wewe ni mwenye kupewa muda (kungojewa)." Surat Al-Hijir aya, 36-37.**

Hivyo "***nadhara***" katika Aya hiyo, maana yake ni kungojea au kusubiri na sio kuona au kutazama. Baadhi ya hao wanaodai kuwa Mwenyezi Mungu ataonekana Siku ya Kiyama wameamini hivyo kwa kutegemea hadithi za Mtukufu Mtume zisemazo kuwa, Mungu ataonekana siku hiyo. Miongoni mwa hadithi hizo ni hadithi isemayo kwamba, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema "Hakika mtamwona Mola Wenu kama mnavyouona mwezi usiku wa mwezi mng'aro."[32] Majibu yetu ni kuwa huko kuchukua mifano ya hadithi kama hizi kunamaanisha kufilisika kidalili. Kwanza, hadithi hizi zimepokewa

31 **Surat Al-Baqarah, aya 280.**
32 *Sahihi al-Bukhari* - kitab attauhiid-Bab Qauluhu Taala Ujuhun Yawmaidhin Nadhirat).

kutoka kwa mtu mmoja;[33] kwa mujibu wa *"Mus-Talahil Hadiith"*. Hadithi za namna hii hufaa kufanyia vitendo, lakini hazifai kuzitumia kwa itikadi kwa vile hazikutokana na hoja za kukinaisha na hasa hasa zinapopingana na hoja za Qur'ani Tukufu kama ilivyo hapa. Hoja hii isemayo kuwa (mtamwona Mola wenu Siku ya Kiyama kama mnavyouona mwezi usiku wa mwezi mng'aro) imetolewa na *Al-Sheikhan*,[34] kutokana na Abu Huraira na Abu Said Al-Khudriy.

Katika *Sahiih Muslim*, imesimuliwa kuwa, Mtume (s.a.w.w.) aliulizwa: "Je, tutamwona Mola Wetu Siku ya Kiyama?" Na akajibu, jee, mnashaka ya kuliona jua mchana pasipo na kizuizi? Wakajibu, "hapana ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu," akasema: je, mna shaka na kuuona mwezi usiku wa mwezi mng'aro pasipo na kizuizi? Wakasema: "hapana ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu." Akasema, basi hivyo ndivyo mtakavyomuona Mola Wenu." Kisha Mtume akaendelea kusema: "Watu wote watakuja siku ya Kiyama kundi moja, kisha (waambiwe) kila umma ufuate unachokiabudu, katika wao kuna watakaolifuata jua, na wengine wataufuata mwezi, na wengine watayafuata masanamu. Kisha ubakie umma huu pamoja **na wanafiki wake,** awajie Mola Wao **kwa sura wasiyoijua** na atawaambia, "mimi ndiye mola wenu" na watamwambia, "tunajilinda nawe kwa Mwenyezi Mungu nasi hatutaondoka hapa mpaka aje Mola wetu. Hapo tena atawajia kwa **sura ile ambayo wanaijua**, aseme "mimi ni Mola wenu", na waseme, "naam wewe ni Mola wetu", kisha watamfuata.[35]

Hadithi hii tumeielewa vyema. Lakini tunawauliza wanaosema kuwa watamwona Mola Wao kwa kufuata hadithi hii kwamba, je, huko

33 Yaani ni Hadithi Ahadi: si mutawatir.

34 Bukhari na Muslim.

45 (i) Tazama (*Sahih Muslim*-kitabul-iyamn bab ithba ruuyatil-muumini-na lirabbihim.) (ii) Au *Sahihi Muslim*-kitabul-iyman, Bab maarifat Tariiq Ruuyat.

kuonekana kwa mola kutakuwa kwa sura (umbo) au si kwa sura? Nimeuliza swali hilo maana niliwahi kusikia wakisema kuwa, watamwona Mola Wao bila ya sura wala umbo! Lau ungechunguza maneno ya hadithi hiyo yasemayo **"BASI HIVYO NDIVYO MTAKAVYOMUONA MOLA WENU,"** yanamaanisha kuwa kama mnavyoliona jua au mwezi ndivyo mtakavyomwona Mwenyezi Mungu; ni wazi kuwa jua na mwezi vyote ni vitu vionekanavyo kwa sura na umbile fulani, iwapo mambo ni kama hayo, basi vipi wanadai kuwa hawatamwona Mwenyezi Mungu kwa umbo maalum?

Ama yale wanayodai badhi yao kwamba makusudio hapa ni kufananisha uoni na uoni: si chenye kuonekana na chenye kuonekana, yanajibiwa na ukweli kwamba ikiwa hoja ni hiyo basi hakuna anayeweza kuliona jua kwa uwazi katika wakati wa jua kali. Ni wazi kwa hivyo, kwamba *tashbihi* (ufananishaji) hii haiko sawa. Vipi isemwe kwamba uoni wetu kwa Allah utakuwa safi kama tunavyoliona jua wakati wa jua kali ilhali wakati wa jua kali huwezi kuliona jua hilo kwa usafi? Hii *tashbihi* si sawa na kama si sawa haya haiwezekani kuwa ni maneno ya Mtume (s.a.w.w.). Kwa hivyo, kwa hali zote mbili, ikiwa kinachofananishwa hapa ni chenye kuonekana na chenye kuonekana chengine (Allah na jua), hilo haliwezekani kwani Allah hana mfano; ikiwa kinachofananishwa hapa ni uoni na uoni mwingine pia haiwezekani kwani uoni mmoja hauko safi kama ulivyodaiwa uoni wa pili. Bali uoni wa jua hauwezekani kabisa kwani hayuko awezae kulitazama katika wakati wa jua kali anga inapokuwa safi.

Suala jingine la kuwauliza ni kuwa, je, Mwenyezi Mungu anageuka kulingana na zama na sehemu tofauti? Au inawezekana kwa Allah kugeuka kutoka hali fulani na kwenda katika hali nyingine? Inapasa tuelewe kuwa kila kigeukacho huwa ni matokeo au kitendo, ama Mungu dhati yake imetakasika na kuwa ni matokeo au kitendo.

Hao wanaodai kuwa watamwona Mola Wao siku ya Kiyama, wameisoma Qur'ani vizuri na kuzifahamu sunna za Mtukufu Mtume kama inavyotakiwa. Na bila shaka wameelewa humo namna gani sifa za Allah zilivyoelezwa kwa uwazi. Je, kutokana na haya anaweza ye yote kati yao akatueleza kwa mujibu wa sifa hizo alizozisoma sura na umbo la Mwenyezi Mungu namna litakavyokuwa siku hiyo ya Kiyama? Na iwapo hataweza kufanya hivyo, maana ya maneno yaliyoko kwenye *Sahiih Muslim* yasemayo: **"Atawajia kwa sura wasiyoilewa,"** na yale **"Kisha atawajia kwa ile sura wanayoifahamu,"** hayatakuwa na maana yoyote. Bila shaka hapana yeyote anayeweza kujibu na kusema kuwa anaweza kuifikiria sura ambayo anataraji kumwona Mola Wake siku ya Kiyama kwa kutegemea yale aliyoyafahamu katika Qur'ani na Hadithi juu ya sifa za Mola Wake.

Usahihi ni kwamba, hapana awezaye kumfahamu Mola alivyo, au kueleza juu ya sifa zake, kisha kwa sifa hizo, akaweza kuhudhurisha picha na sura kamili ya Mola Wake. Kwani Mwenyezi Mungu hawezi kuingia katika mawazo ya Mwanadamu, vitu vingi viingiavyo katika mawazo ya mwanadamu, vitu hivyo huwa ni vitu duni mbele ya Mwanadamu ama Mwenyezi Mungu na Utukufu wake wote tuujuao na ule tusiojua hauwezi kuingia katika mawazo asilan. Ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye anayejijua nafsi yake na alivyo. Na ndio maana Qur'ani ikaashiria hayo kwa kusema: **"Wala wao (Wanadamu) Hawawezi kumjua Mwenyezi Mungu vilivyo."**[36]

Ndugu Mwislamu, hebu sasa linganisha maneno haya ya Mwenyezi Mungu na ile Hadithi inayodaiwa kuwa imesimuliwa na Sahaba Abu Said Al-Khudry (r.a.) na hapa tunainukuu kipande chake cha mwisho: "Na Mwenyezi Mungu atawajia waislamu kwa sura iliyo kinyume na sura waliyoiona mwanzo, hapo Waislamu waseme twajilinda nawe,

36 **Surat Taha aya ya 110**.

wewe si Mola wetu, nasi hatutaondoka hapa hadi atujie Mola wetu."[37] Hebu sasa linganisha maelezo ya mwanzo ya Siku ya Kiyama kama yalivyoelezwa na hadithi zilizoko kwenye *Sahih Muslim*. Lakini je, waumini walikwisha kumwona Mola Wao hapo mwanzo hadi waseme watakapomwona asiyekuwa Mungu: "Twajilinda nawe, wewe, si Mola wetu?" Na kama walimwona hapo mwanzo walimwonea wapi? Na je Mwenyezi Mungu anabadilika sura hii na ile: kubwa na ndogo?!

Miongoni mwa madai ya madhehebu la *Ahlul Sunnah wal jama'ah* ni kuwa kumwona Mungu ni neema kubwa watakayoipata Waislamu wacha Mungu tu yakiwa ni malipo kwa matendo yao mema duniani huko Akhera; lakini kwa mujibu wa hadithi hiyo tuliyotangulia kuitaja, Mtukufu Mtume ameeleza kuwa wanafiki na Waislamu wa Umma huu wote watakuwa pamoja wakimngojea Mola Wao na ndipo, eti, Mola Wao awajie kwa sura wasiyoijua na baadae sura wanayoijua. Hivyo Hadithi hii inapelekea kufahamika kuwa wanafiki na watu wema watashirikiana katika kumwona Mungu (swt.), na hilo ni jambo lisilowezekana kwa mujibu wa itikadi waliyonayo. Nakukumbusha kuwa kwa mujibu wa itikadi ya *Ahlul-Sunnah*, watakaomwona Mungu ni waumini tu pekee yao, sasa itakuwaje hadithi hii iwaingize hata wanafiki?

Katika mjadala huu wa kihistoria na kutaka kuthibitisha zaidi imani yao ya kuonekana kwa Allah kwa macho ya utosini, kuna waliodai kuwa Mwenyezi Mungu ataonekana huko Akhera kwa kutumia ushahidi na ufahamu wa aya:

37 *Sahiih Muslim*-Kitab-lyman-bab, Ithbat-Ruuyatil Muuminin Lirabbihim. (Hadithi nambari 299 au 296).

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 27



﴿ ۞ لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا۟ ٱلْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ ۖ ﴿٢٦﴾ ﴾

**"Wale waliotenda wema watapata (Jaza) ya wema na ziada" Surat Yunus aya ya 26**.

kama ni aya iliyothibitisha kuonekana kwa Allah huko Akhera. Wakafahamu kuwa maana ya **wema** katika aya hii ni pepo na maana ya ziada ni **- kumwona Mwenyezi Mungu!!**

Jambo hili si kweli na wala neno *ziada* lililoko kwenye aya hiyo ya 26 ya **Sura Yunus** halina maana hio wala muradi wake si kumwona Mungu. Hiyo ni ishara ya kupata malipo mengine ya ziada katika malipo ya peponi, kama kupandishwa daraja ndani ya pepo, maana pepo nayo ina daraja na tabaka tofauti kwa kutegemea ibada na wema wa Mwislamu. Na utapoichunguza aya hii kwa makini utakuta kuwa maelezo haya tuliyoyatoa ndio hasa kusudi la aya hiyo. Kwani baada ya Mwenyezi Mungu kusema: **"Wale waliotenda wema watapata *(jaza)* yao wema na ziada,"** Mwenyezi Mungu hakuishia hapo bali ameendelea kuwapamba waumini kwa sifa nyingi zenye kuonyesha maana hasa ya ziada yenyewe kwa kusema mbele ya aya hiyo hiyo, **"na wala nyuso zao hazitakuwa na weusi wala hazitakuwa nyonge."** Maneno yanayomaanisha kuendelea kwao kupewa neema na rehema na kuzidishiwa neema hizo za peponi muda baada ya muda. Kwa maana hizi nyuso zao hazitakunjana wala kudhalilika. Ama katika aya ya 27 ya **Surat Yunus** hiyo hiyo, Mwenyezi Mungu amewazungumza vingine watu wabaya na akasema: **"Na wale waliochuma mabaya watalipwa ubaya na watakumbwa na udhalili, hawatakuwa na mtetezi mbele ya Allah."** Yote hayo yanamaanisha kutopata kwa Utukufu kwa watu wabaya maana watalipwa UBAYA ambao maana yake ni MOTO na watakuwa wanyonge (dhalili) na hatimaye watakosa mtetezi. Kwa maana hii, katika moto

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 28



hakutakuwa na nafuu, bali kila uchao ni adhabu na unyonge usio na mwombezi. Ama, katika pepo kila siku kutakuwa na ziada katika neema hizo zilizoandaliwa na Allah peponi. Na kila siku watakuwa wanafaidika na kuneemeka kwa neema za Allah zilizo mpya kwao. Hivyo, neno 'ziada' halimaanishi ''**kumuona Allah'** kama wanavyodai.

Hadithi nyingine inayotegemewa na wafuasi wa Muhammad bin Abdul-Wahhab ni ile isemayo: "Watakapoingia Waumini peponi, Mwenyezi Mungu atawaambia: Je, mnataka chochote cha ziada nikuzidishieni? Watasema: Kwani hukuzifanya nyuso zetu kuwa nyeupe? Kwani hujatuingiza peponi na ukatuepusha na moto?"

Kisha pataondolewa kizuizi *(hijab)*, na watamwona Mola Wao, na watakuwa kama hawakupewa lolote, la kuwapendeza na lililo bora kuliko huko kumtazama Mola Wao."[38] Katika hadithi hii:

Kuonekana kwa Mungu kunafahamika kuwa kutatokea baada ya waumini kuingia peponi.
Kwa mujibu wa hadithi ya Abu Hurayra na ya Abu Said Al-Khudry ambazo wengi wa Waislamu wanazitegemea, kuonekana kwa Mungu kumeelezwa kuwa kutatanguliwa na kuonekana kwake kabla ya kuingia kwa waumini peponi!

Katika Hadithi hii kumuona Allah ndio malipo makubwa yao.

Katika Hadithi zilizotangulia, wanafiki nao pia watamuona!
Yote hayo yanathibitisha kwamba kuna tofauti na kutokubaliana katika riwaya hizi na wala hapana kimbilio la kuepukana na maelezo

38 (i). *Sahiih Muslim* - Kitabul Iyman. Bab Ithbat Ruuyatil Muuminiin Fil Akhirat Rabihim. Hadithi nambari 297. AU (ii). *Sunan Ibnu Majaa*, Kitabul-Muqadimat, mlango uitwao Bab Ma Ankarat Aljahmiyyat. Hadith nambari 184.

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 29



yenye kupingana na riwaya hizi isipokuwa kuungama na kukubali kuwa huko kuonekana kwa Allah maana yake ni kuzidi kupata maarifa ya Mwenyezi Mungu baada ya kupata malipo. Wanaodai kuonekana kwa Mungu hawakuishia hapo bali wamezua dai jingine, nalo ni kuwa Mtukufu Mtume, eti, alimwona Mola Wake katika usiku wa Miiraj! Huu ni uzushi mwingine usio na asili yoyote katika Uislamu. Mtume Muhammad (s.a.w.w.) hakumwona Mola Wake kwa macho bali moyo wake ndio uliona ishara na alama za Mwenyezi Mungu. Qur'ani kuhusiana na mnasaba huu imesema yafuatayo: (Moyo wa Muhammad haukuongopa kuhusiana na yale uliyoyaona. Kwa hakika aliona (Muhammad) alama na ishara za Mola Wake zilizo kubwa). **Surat An-Najmi aya ya 18.**

Aya hizi ni katika aya zilizozungumzia Miiraj ya Mtume na wala hazijasema kuwa Mtume alimwona Mola Wake. Bali lililo mashuhuri kutokana na aya hizi ni kule Mtume kuona miujiza na ishara za Mola Wake kama aya zilivyoashiria. Kwa kuwa Mtume hakumwona Mola Wake wala yeye mwenyewe hakusikika kudai hayo, madai yaliyo kinyume na hayo ni makosa na uzushi usiokuwa na asili katika Uislamu. Aya nyingine wanayoitegemea baadhi ya maulamaa wa Kiwahabi kuthibitisha dai la kuonekana kwa Mungu ni aya *"Qala Innahum An Rabihim Yawma Idhi Lamah Juwboon"* maana yake sahihi si kama (Makafiri watazuiliwa na kumwona Mola Wao) kama wanavyodai wengine, bali maana sahihi ni kwamba:**"Hakika watazuiliwa, siku hiyo na (neema) za Mola."**[39]

Aya hii yaonesha kule kuzuiliwa kwa makafiri na wanafiki kupata neema na rehma za Mwenyezi Mungu na sio kuzuiliwa kwa makafiri na kumwona Mwenyezi Mungu. Bali aya hii imefasiriwa na aya iliyoko katika **Surat Al-Hadiid** na hapa nainukuu:

39 **Al-Mutaffifyn aya ya 15.**

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 30



﴿ يَوْمَ يَقُولُ ٱلْمُنَٰفِقُونَ وَٱلْمُنَٰفِقَٰتُ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱنظُرُونَا نَقْتَبِسْ
مِن نُّورِكُمْ قِيلَ ٱرْجِعُوا۟ وَرَآءَكُمْ فَٱلْتَمِسُوا۟ نُورًا فَضُرِبَ بَيْنَهُم بِسُورٍ لَّهُۥ
بَابٌۢ بَاطِنُهُۥ فِيهِ ٱلرَّحْمَةُ وَظَٰهِرُهُۥ مِن قِبَلِهِ ٱلْعَذَابُ ﴿١٣﴾ ﴾

**“Siku watakaposema wanafiki… ‘tungojeeni ili nasi tupate mwangaza katika nuru yenu.’ Waambiwe, ‘rudini nyuma mkatafute nuru yenu ‘uwekwe baina ya (wanafiki na waumini) ukuta wenye mlango, ndani yake mna rehema na nje kwa upande wake wa mbele kuna adhabu.” *(*Al-Hadiid: 13).**

Hivyo, ukuta huo ambao umetajwa katika Sura hii ndio ule ulioelezwa kwa jina la Hijab katika **Surat Al-Mutaffifyn.** Hivyo, kizuizi kikubwa kitakachowekwa baina ya makafiri na Mwenyezi Mungu ni kule kukosa rehema na amani ya Mwenyezi Mungu huko Akhera. Kwa sababu Waumini wao ni wapenzi wa Mungu, wao hawatawekewa kizuizi cha aina yoyote bali watapata rehema na amani ya Mungu isiyo na mwisho. Neema hizi za Mungu watakazozipata Waislamu hazina mwisho wala hazitapunguzwa, maana ndio hasa zawadi aliyoiandaa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Waislamu peponi. Hayo ni kama yale yaliyothibitishwa na **Surat Huud** aya ya 108. Neno hili Hijab, lililotajwa kwenye aya ya 15 ya **Surat Mutaffifyn** halimaanishi kutoonekana kwa Mungu na makafiri bali linamaanisha kizuizi kitakachowekwa baina ya makafiri kama ilivyo kwenye aya ya 13 ya **Surat Hadid**. Kwa maana hiyo, makafiri watatengwa na waumini, hayo pia utayapata katika aya, “**Wabaynahuma Hijab,”** ‘na baina yao kutakuwepo na kizuizi’’**Surat Aaraf aya ya 46.**

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 31



Hivyo, kuihusisha aya hii na kuonekana kwa Mungu huko Akhera na Waislamu ni jambo lisilo na msingi. Pili: Ni kuwa hata ingelikuwa kweli maana ya hijabu (kizuizi) kilichotajwa katika **Surat Mutaffifyn** kina maana ya kuwazuia Makafiri kutokana na kumuona Mwenyezi Mungu, basi kuthibitisha kumuona kwa Aya hii itakuwa ni kwa ile njia iitwayo **mafhumu Al-Laqab.** Yaani itakuwa na maana kwamba iliposemwa kuwa "Hawa hawamuoni" wao wakadai kwamba "Basi hawa watamuona." Na *mafhumu Al-Laqab* haikubaliki hata katika mas'ala ya fiq'hi ya ijtihad, basi vipi itakubalika katika itikadi?! Haya yote ni kwa kujaalia tu, vyenginevyo aya hiyo haina maana ya kuwa makafiri watakuwa hawamuoni Allah, bali watazuiliwa kutokana na rehema Yake.

Kadhalika wenye dhana ya kumwona Mungu huko Akhera pia wameitumia aya: **"Mola wangu! Nioneshe (Nafsi yako) ili nikuone."[40]** Wakasema kuwa, laiti ingekuwa kumwona Mungu ni muhali Mtume Mussa (a.s.) asingeyaomba hayo maana yeye anajua zaidi lililo muhali na lisilo muhali. Kauli yao hii haina ukweli hata kidogo. Na wala Mtume Musa hakuyaomba hayo kwa ajili ya nafsi yake, bali aliyaomba baada ya Bani Israil kuyataka hayo. Angalia aya: **"Na kumbukeni mliposema, ewe Musa, hatutakuamini mpaka tumwone Mwenyezi Mungu wazi wazi."[41]** Kwanza, aya inadhihirisha kwa uwazi kuwa ni mayahudi waliotaka kumwona Mungu lakini kwa sababu Musa ndiye Kiongozi wao, ni lazima yeye awatekelezee maombi yao kwa Mungu na lengo la Nabii Musa ni kutaka waelewe ya kuwa Mungu haonekani. Na ili awapatie adhabu kutoka kwa Mungu, angalia adhabu iliyowapata Mayahudi baada ya kusema hayo kwenye mwisho wa aya hiyo ya 55 ya **Surat Al-Baqarah .**

40 **Aaraf: 143.**

41 Aya ya 55 ya **Surat al-Baqarah**.

Pili: Ni kuwa ombi hili la Musa ni sawa na ombi au maneno ya Ibrahim (a.s.). Ibrahim (a.s.) hakuwa mjinga wa kutojua kuwa Mwenyezi Mungu ni tofauti na viumbe vyake, lakini pamoja na hayo alipoona nyota akasema: **"Huyu ni Mola wangu",** na alipoona mwezi akasema: **"Huyu ni Mola wangu",** na alipoona jua akasema: **"Huyu ni Mola wangu. Huyu ni mkubwa zaidi."** Bila shaka Nabii Ibrahim (a.s.) aliyasema hayo ili awalaumu na kuwaita katika ukweli watu wake ambao wakiabudu nyota na kuvitukuza viumbe vya angani. Alitaka awaongoze kwenye haki na kuwafahamisha kuwa kila kinachopotea (kuja na kuondoka) hakileti maana ya uhakika wa Mwenyezi Mungu wala hakistahili kuabudiwa, maana mwabudiwa huwa na sifa maalumu na sifa hizo zinaeleweka na kila Mwislamu, nazo ni kinyume na sifa za nyota, mwezi na jua, au za viumbe wengine.

## KUMTAKASA MWENYEZI MUNGU

Mwenyezi Mungu lazima atukuzwe na kutakaswa na hii *(Tauhid)* ndio nguzo muhimu kabisa katika Uislamu. Kuamini Mwenyezi Mungu wa pekee ni jambo kubwa ambalo Mwislamu litampelekea kupata radhi za Mola Wake. Kwa sababu ya kuelewa umuhimu wa *"Tauhiid"* maadui wa *Tauhiid* wamejaribu kama walivyoweza ili wawapoteze Waislamu na hatimaye wawaweke mbali na *Tauhiid*. Mwenyezi Mungu amesifiwa kwa kila aina ya sifa nzuri na Qur'ani inashuhudia sifa za Mola kila uchao na sifa hizo zinaeleweka na kila Mwislamu. Lakini wakorofi hamu yao kuu ni kuwapoteza Waislamu. Ndio maana wamezua mengi kuhusiana na Allah, Mtume, na hata ibada. Ndugu Waislamu, miongoni mwa sifa na hali zinazomstahikia Mwenyezi Mungu kama alivyosifiwa na Uislamu sahihi, ni kutokuwa na mwili, kutokukaa, kutokuteremka; haonekani na macho; na sifa nyinginezo. Hivyo elewa ewe Mwislamu ya kwamba Uislamu hause-

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 33



mi kama walivyosema *Al-Hashwiyya Al-Mujassima”*, ya kwamba Mungu ana kiwiliwili na kwamba ataonekana, kwa kusema hayo wamepinga aya ya Qur’ani isemayo:

**لا تُدْرِكُهُ الأَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الأَبْصَارَ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ“**

*Laa tudriquhul-Absar Wahuwa Yudriqul-Absar”*

aya hii inakataa kinaga ubaga kule kuonekana kwa Mwenyezi Mungu na macho ya viumbe. Pia *Ashaira* na Hashwiyya wamekataa kauli ya Mwenyezi Mungu kwa Nabii Musa (a.s.) isemayo, **“LAN TARANI”** “Hutaniona” inayomaaanisha kutowezekana kuonekana Mungu kwa Macho milele. Kutokana na udhaifu wa dalili wamedai kuwa neno *“Lan”* lamaanisha kutowezekana kuonekana kumwona Allah duniani tu, basi nini maana ya neno *“Lan”* lilioko kwenye aya ya **Surat Baqarah** isemayo *“Wa**<u>lan</u>** Tafa-aluu”*, yenye maana “na hamtoweza kufanya” jee itamaanisha duniani tu? Na kwamba endapo Mungu angewataka makafiri wa Kikuraishi walete mfano wa Sura moja ya Qur’ani siku ya Kiyama wangeleta? “Hasha”, hilo halitawezekana asilan. Ukweli ni kwamba Mungu haonekani na jicho la mwanadamu yeyote Duniani wala Akhera.

Angalia madai ya kutaka kumwona Mungu yameitwa kuwa ni dhulma, Mwenyezi Mungu amezungumza habari ya Bani-Israil na Musa (a.s.) kwa maneno yafuatayo:-

**فَقَدْ سَأَلُوا مُوسَى أَكْبَرَ مِنْ ذَلِكَ فَقَالُوا أَرِنَا اللَّهَ جَهْرَةً فَأَخَذَتْهُمُ**
**الصَّاعِقَةُ بِظُلْمِهِمْ**

***Faqad Saalu Musa Akbaramin Dhalik Faqalu Arina Llaha Jaharata Fa-a Khadhathumu Swa’iqatun Bidhulmihim”***

**"Hakika walimwomba Mussa makubwa mno kuliko hayo, walisema tuonyeshe Allah tumwone kwa dhahiri, wakaangamizwa na adhabu kwa dhuluma yao".**[42] Laiti kumwona Mungu inawezekana, basi Mwenyezi Mungu asingeyaita madai ya kutaka kumwona kuwa ni dhuluma inayostahili adhabu waliyopewa.

Hivyo, wanaodai kuwa Allah ataonekana kwa macho au huonekana kwa macho wamejivika itikadi hiyo ya kumwona Mwenyezi Mungu ambayo wameichukua kutoka kwa Dini za Mayahudi na Manasara.

Kwa kuwa Tawhiid ni muhimu kwa kila muumin sisi Waislamu hatutakubaliana daima na mawahabi wanaoipinga Qur'ani dhahiri shahiri. Kwa upotevu wao wanamthibitishia Allah kuwa na viungo kama vile masikio na mikono. Itikadi hii mmeipata wapi nyinyi Waislamu wa Afrika. Ama Mawahabi inaeleweka walipoipata, wameipata itikadi hiyo kwenye dini ya mababu zao Mayahudi, ambao maisha yao yote waliyamaliza kwa kudai kutaka wamwone Mungu. Ndugu msomaji, angalia kwa makini, haifai wala hatuwezi kumthibitishia Allah ambaye ndiye aliyetuumba, kuwa na mwili. Inaeleweka wazi kuwa mara tu unapomthibitishia Allah mikono, macho na masikio ni tayari umeshampa umbo maalum ingawa wajitia hamnazo kwa kusema umbo hilo *Yaliqu Bijalalihi*, yaani umbo, "Linalomstahikia yeye Mwenyezi Mungu katika utukufu Wake!!

Tunapenda ifahamike kuwa laiti Allah angekuwa na mikono miwili kama wanavyodhani baadhi ya waislamu, asingejisifu pia kwa sifa ya kuwa na mikono mingi zaidi ya miwili kama alivyosema, Sura ya 51 aya ya 47:

﴿ وَٱلسَّمَآءَ بَنَيۡنَـٰهَا بِأَيۡيْدٍ وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ ﴿٤٧﴾ ﴾

**"Na Mbingu tumezijenga kwa Mikono (ayd), na hakika tutazitanuwa ziwe pana." An-Nisaa 153**

**42 Sura An-Nisaa 153**

**ya** Pia Allah amemsifu mja wake Nabii Daudi kwa sifa hiyo hiyo ya kuwa na mikono mingi zaidi ya miwili kinyume na ilivyo kawaida ya mwanadamu kwa kusema katika Sura ya 38 aya ya 17:

"Kuwa na uvumilivu kutokana na wanayoyasema, na mkumbuke mja wetu Daudi mwenye mikono mingi; kwani yeye siku zote ni mnyenyekevu kwetu."

Tanbih: Wote Allah na Nabii Daud (a.s) wamepewa sifa ya kuwa na mikono zaidi ya miwili basi laiti kuwa sifa hii ni ya uhakika kama wanavyodai wenye kuitakidi kuwa allah ana mwili, tungelazimika pia kukubali kuwa mikono ya Allah na ile ya Daudi ni zaidi ya miwili kwani lugha iliyotumika ni ya "Uwingi, "*plural form*" lakini haya yanathibitisha kuwa Allah kwenye aya hiyo amekusudia kujisifu kwa sifa ya nguvu nyingi na pia kumsifu mja wake Daudi kwa sifa hiyo hiyo, tofauti iliyopo kati yake *Subhanahu wataala* na huyo Daudi ni kuwa aya inayomsifu Allah, inazungumzia uweza Wake wa kuumba kwa Mbingu na kuzitanua, amma sifa ile ya Daudi inamsifu kwa nguvu zake za kimwili na ushujaa wake katika utawala wake na unyekekevu wake kwa Allah. Na jambo hili liko wazi kabisa kwa kila mwenye akili na maarifa timamu ya elimu ya theolojia na Tawhid sahihi.

Basi naifahamike kuwa, neno *Yad*, ambalo lina maana ya mkono katika lugha ya Kiarabu lakini baadhi ya wanaodai kuwa Allah ana viungo pia wamelipotoa katika Qur'ani kwa dhana zao za kijahili kuwa eti Allah naye ana mkono! Hapana, neno *Yad* linapotumika kwa Mungu (**asiyehitajia kuwa na mkono wala viungo**) haliwi na maana ya mkono, kama vile neno "*Mattar*" ambapo linaponasibishwa na adhabu itokayo juu huwa halina maana "ya *mvua*" bali lina maana ya "*adhabu.*" Angalia aya, "*Waamtarna Alayhim Matara*" **(aya ya 84 Surat al A'araf)** pia jaribu kuelewa kuwa neno **"RIIH"** katika Qur'ani halikuja kwa maana ya '*upepo*' tu peke yake, bali bia "ni

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 36



adhabu," dhoruba, na maangamizo ama neno hili hili linapokuja kwa namna ya wingi, yaani **"RIYAH"** huwa lamaanisha "Mvua" angalia aya isemayo *"Watasrifu Riyah"* au *"Yurssilu Alayqum Riyah"* neno *'Riyah'* kiistiari katika Qur'an ni 'mvua.'

Na lau ilikuwa mkono na uso na mengineo yamekusudiwa maana yake ya uhakika kwa msingi wa kukataa *majazi*, basi Mawahabi itabidi waseme kwamba hio mikono ya Mungu, miguu yake, macho yake na masikio yake, yote yataangamia na Mungu hatobaki isipokuwa uso wake tu kwani hivyo ndivyo Qur'ani inavyosema. Anasema Allah: كل شيْء هَالكٌ إلا وَجْهَه "Kila kitu kitaangamia isipokuwa USO Wake". Na pia amesema: كل مَنْ عَليْهَا فان وَيَبْقى وَجْهُ رَبِّكَ (Kila kilichopo juu yake (mgongo wa ardhi) kitaakwisha. Na utabakia USO wa Mola Wako…." Kwa hivyo, hio itikadi ya kuwa Mungu ana uso na macho na mengineo, msingi wake ni ujinga wa Kiwahabi wa kutokuifahamu vyema lugha ya Qur'ani.

Kwa mujibu wa Madhehebu ya Kiwahabi Mwenyezi Mungu huwa na mikono, macho na hata miguu, *Subhanallah!* Usishangae hayo wameyathibitisha wenyewe katika vitabu vyao walivyoviandika kwa kuwahadaa Waislamu. Katika sehemu hii tutaeleza zaidi sifa za Mwenyezi Mungu aliye Mmoja kama itikadi yetu inavyosema. Nayo ni kwa mujibu wa Qur'ani Tukufu na Sunna za Bwana Mtume (s.a.w.w.). Maana sisi hatuelezi lolote kwa akili zetu ni lazima tutegemee Qur'ani na tutegemee Ushauri wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hivyo, Mwenyezi Mungu ni Mmoja asiye na Mshirika wala aliyefanana naye wala hana mwili wa aina yoyote haiwezekani kwake kuonjwa, kuonwa na kugunduliwa kwa njia ya hisia za kimaada. Yeye ametofautiana na maada (*material*), hivyo hawezi kuchukua nafasi wala kujiingiza kwenye umbo lingine linaloishi. Ni muhali kwake kuwepo sehemu fulani na akakosekana kwingine. Macho hayamwoni Allah bali yeye huwaona wenye macho. Wala haisihi kusemwa, yuko

wapi Mungu? Au kusemwa, yukoje Mungu? Kwa sababu masuala haya, yu wapi, na yukoje hutumika kuulizia yule au kile, chenye umbo fulani na kukosekana kwenye sehemu nyingine. Na yote hayo hayastahiki kwa Mwenyezi Mungu ambaye ni Muumba wa maumbile na mletaji wa hizo sehemu ambazo wajinga wanamnasibisha nazo. Tunarejea kusema kuwa Mwenyezi Mungu alikuwepo kabla ya kuumbwa kwa nyakati, mahala na zama naye hajabadilika wala habadiliki.

Kwa mujibu wa itikadi ya Uislamu, ni kuwa hata hizo aya zilizotajwa na kumaanisha dhahiri ya kuwa Mungu amejisifu kwa sifa ya uso, mkono, na kwamba ana sifa ya kukaa *(al-istwaa)*, zote hizo ziko katika fani ya majazi iliyotumika kwa maana isiyo ya dhahiri. Wala Muislamu yeyote hawezi kukana ya kuwa katika Qur'ani mna lafudhi zilizotumika kwa njia ya "Majazi." Lafudhi za majazi pia zimetumika katika hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na hata katika maneno ya watu wa Fasihi ya lugha ya Kiarabu. Kwa kudai kwamba Mungu ana uso na muundi wa mguu na kumpa sifa ya *istwaa* kwa kumaanisha kuwa sifa za dhahiri ni kuamini kuwa Mungu ana kiwiliwili na kwamba analazimika kuhitajia viungo vyake! Itikadi hii ya Mungu kuwa na viungo na mwili unaomstahikia yeye Mwenyezi Mungu katika utukufu wake ndiyo itikadi ya *Salafiyyah* na wachache wenye kuwaunga mkono katika *Ahlul-Sunna*, Hashwiyya, Mujassima. Lakini juu ya hayo hawajaepukana na kumpa Mungu mwili ingawa wanadai kutojua *Kayfia (*namna*)* yake, na kwamba mwili huo unamstahikia yeye tu kwenye Utukufu Wake! Ni makosa kusema kama wanavyosema mawahabi ya kuwa, Mungu huteremka inapobakia theluthi ya mwisho ya usiku akaja kwenye Uwingu wa dunia, akanadi akisema, Je, yuko mwenye ombi nimtekelezee? Yuko mwenye kutaka msamaha nimsamehe? Ikiwa Mungu anapanda na anashuka na kwamba madhumuni ya kutenda hayo ni kuja kuongea na waja Wake na kuwarehemu, basi lini Mungu alikosekana katika

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 38



dunia hii mpaka tuambiwe huja usiku hata usiku?

Cha kuchekesha ni kuwa utawasikia wafuasi wa Salafiyyah wenyewe kwa wenyewe wanatofautiana: Je Mungu akiondoka kuja mbingu ya kwanza ile Arshi (kiti cha enzi) huiacha tupu? Wengine huona kuwa anaiacha tupu! Wengine husema kuwa huja umbingu wa kwanza na kule yuko. Sasa tunawauliza huyu Muungu wao anapanda na kushuka kwa kuhitajia nini, kwani asipopanda na kushuka ni nini atakachokikosa kwenye utukufu Wake? Pia natujiulize je kwani Mungu anaogopa kuja Duniani mchana? Hii kama si kufuru wala basi hatuoni kuwa ni katika imani. Na Mungu anahitajia nini mpaka apande na kushuka? Kwani ameshindwa kutenda alitakalo mpaka ashuke? Yeye ni *"Faalun Lima Yuriid"* (mwenye kutenda alitakalo), na kwamba anapotaka kuumba ama kuleta jambo lolote, husema "kuwa" na mara huwa. Lini Mungu alihitajia mkono, uso au macho natuache mzaha; kwa kufuata mwongozo wa Mtume Muhammad mambo haya hayakumstahikia Mwenyezi Mungu. Enyi ndugu zangu Waislamu natujifunze kumtakasa Mwenyezi Mungu kama Qur'ani inavyotuagiza.

Twasema kuwa, kauli zao hizi za kutozifanyia *taawil (maana ya uhakika)* aya za Qur'ani na kuzipa tafsiri inayomtakasa Mungu na Dhati Yake ili asiwe na mwili ama viungo ni itikadi potofu. Angalia hata katika lugha yetu mtu akisemwa kuwa "**ana mkono**" humaanisha kuwa mtu huyo ni mwizi. Inaposemwa kuwa *"mpenda chongo huona kengeza"* humaanishwa kuwa, *"mtu hukithamini anachokipenda."* Isemwapo *"fulani ana kijicho"* humaanisha kuwa *"mtu huyo ana choyo."* Na inaposemwa kuwa *"ana ulimi"* humaanishwa kuwa mtu huyo ana tabia ya "kutukana" au *"kutokuheshimu"* watu. Ndugu Waislamu, tujihadhari sana na watu wanaotaka kuondoa fani hizi za kuielewa Qur'ani, Mwenyezi Mungu mwenyewe amesema katika Kitabu chake Kitukufu:

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 39



﴿ إِنَّآ أَنزَلۡنَٰهُ قُرۡءَٰنًا عَرَبِيّٗا لَّعَلَّكُمۡ تَعۡقِلُونَ ٢ ﴾

*"Inna anzalnahu Qur'anan Arabiyan la'alakum ta'aqilun".*

**"Hakika tumeteremsha Qur'ani kwa lugha ya Kiarabu ili mpate kufahamu".Surat Yusuf Aya ya 3**

Ni jambo la kawaida kuwa haitawezekana kuilewa Qur'ani vizuri mpaka uzisome fani za lugha ya Kiarabu. Waarabu pia wamesema kwa *majazi* na kwa *hakika* na pia husema kwa *istiara*. Na tutakapokataa kuwa Qur'ani haina fani hizi, huko ni kuitoa Qur'ani katika lugha ya Kiarabu baada ya Allah kwisha kuthibitisha kuwa Kitabu Chake amekizungumza kwa maneno na lugha ya Kiarabu. Ndugu Waislamu, angalieni mtaona kuwa vitabu hivi ni vingi vinavyoandikwa lakini jihadharini sana na watu ambao nia yao kubwa ni kuikebehi na kuipinga Qur'ani. Majazi katika Qur'ani imekuja katika aya nyingi, mfano wa hayo ni aya ya 82 ya Surat Yusuf isemayo:-

وَاسْأَلْ الْقَرْيَةَ الَّتِي كُنَّا فيهَا وَالْعيرَ الَّتِي أَقْبَلْنَا فيهَا

*"Fas'alul Qariata Latii kunna Fiyhaal Wal Iyra latii Aqbalna fiha."*

"Na uulize mji tuliokuwa na msafara tuliouona."

Angalia, kuuliza mji ni kuwauliza *wakaazi* wake na kuuliza msafara ni kuwauliza wenye msafara lakini neno *"wakaazi"* na neno *"wenye msafara"* halionekani katika **Surat Yusuf**. Hiyo yote inathibitisha kujuzu kusema au kutumia lugha kama hiyo. Hivyo neno ***Yad*** (mkono), *Jaa Rabbuka* (kuja kwa Mola) na kushuka kwa Mola, yote haya yamekuja na kutumika kwa njia ya *majazi* na sio dhahiri. Na maana sahihi ya mkono wa Mwenyezi Mungu inapatikana kwa mujibu wa Qarina (*context*) na *siyaq.*

Wakati mwengine hufasirika neno ***yad*** kwa maana ya Qudra na Uweza; wakati mwengine kwa maana ya nguvu; wakati mwengine kwa maana ya *mubashatu Al-Fi'il biduni wasatiyya* (kumaanisha kuwa Allah mwenyewe ndio mtendaji pasi na aliyeingia kati); wakati mwengine kwa maana ya kuunga mkono. Na maana hizi zote zimepokewa katika lugha ya Warabu. Ama kuja Kwake ni kuleta rehema Zake au adhabu Zake, au amri Zake. Kama alivyosema hayo Mwenyewe Mwenyezi Mungu katika Qur'ani:-

فَأَتَى اللَّهُ بُنْيَانَهُمْ مِنَ الْقَوَاعِدِ فَخَرَّ عَلَيْهِمُ السَّقْفُ مِنْ فَوْقِهِمْ

**"Mwenyezi Mungu akazijia nyumba zao kwenye misingi, dari zikawaangukia juu yao."**

Je hapa Mungu pia alikuja akaingia kwenye misingi ya nyumba kisha akaziporomoa?! Kwa hivyo, kwa vile kitu bora cha kuifasiria Qur'ani ni Qur'ani yenyewe, basi sisi tunazirejesha Aya kama hizo katika Aya kama: أَتَى أَمْرُ اللَّهِ ***"Ataa amru llah"*** (amri ya Mungu imekuja), na aya kama: فتربّصوا حتى يأتيَ اللهُ بأمْره ***"Fatarabbasu hata ya-atiya llahu biamrihi"*** (Basi ngojeni mpaka Mungu alete amri yake). Hivyo aya *Wa jaa rabbuqa"* muradi wake ni kuja na kufika kwa amri ya Mola. Neno amri katika *"wa jaa Rabbuka"* ni *"Mukaddarah" (*lililokadiriwa tu kuwepo kwake*)*. Hayo ni kwa kuwa Mungu hateremki kwa sababu hakuna masafa kati ya jambo lolote na Mungu Subhanahu wataala. Hivyo ndivyo Qur'ani ilivyotuashiria, *'Ata amrullah,'* (amri ya Allah ni yenye kuja). Katika kuamuru kutazama mara nyingi Allah huamuru watu kutazama vile vyenye umbo na mwili hayo ni kwa sababu kuamuru macho kutazama kitu kisicho na umbo ni jambo lisilowezekana. Kwa mfano Qur'ani inatuamuru tutazame ngamia, mbingu, ardhi, kwa kutumia

sentensi " *Afala yandhuruuna ilal….*"[43] Jambo ambalo linathibitisha kuwa neno "*nadhira*" au "*yandhuruun*" linapofatana na kitu chenye mwili na umbo ama chenye kuchukua nafasi itamaanisha kutazama.

Amma neno "*nadhira*" lilioko katika **Surat Al-Qiyamat**, halimaanishi kuona au kutazama Dhati ya Allah, na hasa kwa vile Allah hana umbo maalum litalowezesha macho haya kumwona yeye. Na huko kutajwa kwa nyuso katika Qur'ani kuna maana kubwa kabisa, mara nyuso hizo huelezwa kuwa zimedhalilika na mara husemwa kuwa zimenawiri na kung'aa. Yote hayo yanathibitisha kuwa nyuso zitazong'aa zitakuwa hivyo na hatimaye kunawiri kutokana na furaha ya vile vilivyoonwa na macho yao navyo ni "chemchemu zenye kutiririka, vitanda vilivyonyanyuliwa juu, vikombe na gilasi zilizowekwa tayari kwa kutumiwa na wao, mito ya kulalia (*pillows*) iliyopangwa na hatimaye mazulia yaliyotandikwa vyema.[44]Qur'ani Tukufu katika kueleza yale yatayotazamwa na macho ya waumini ikaendelea kutueleza hivi: **"Hakika ya watu wema watakuwa katika neema watakuwa juu ya mali wanatazamana. Utaona kwenye nyuso zao mng'aro unaotokana na neema (hizo).**[45] Kwa maana hii, twaelewa kuwa kutazama huku kulikotajwa na aya ya 23 kunamaanisha kwa waumini hizo neema kubwa na maandalizi mazuri walioandaliwa na Mola Wao. Aya ya 24 isemayo kuwa "utaona kwenye nyuso zao mng'aro wa neema" ni kithibitisho kikubwa kuwa waumini hao watakuwa hawamtazami Mola Wao bali wanazitazama neema alizowapa wakiwa juu ya vitanda ama viti vyao huko peponi. Hayo yanathibitishwa zaidi na aya zile zinazotaja kudhalilika kwa nyuso nyingine. Aya hizo mara nyingi hueleza kama ifuatavyo.

43 **Surat al-Ghaashiya: 17-20**

44 Tazama, Sura 88, **Surat Al-Ghaashiya**, aya ya 8-16.

45 Sura ya 83, **Al-Mutafifyn**, aya ya 22-24.

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 42



﴿ وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ خَاشِعَةٌ ﴿٢﴾ عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ﴿٣﴾ تَصْلَىٰ نَارًا حَامِيَةً ﴿٤﴾ تُسْقَىٰ مِنْ عَيْنٍ آنِيَةٍ ﴿٥﴾
لَّيْسَ لَهُمْ طَعَامٌ إِلَّا مِن ضَرِيعٍ ﴿٦﴾ لَّا يُسْمِنُ وَلَا يُغْنِي مِن جُوعٍ ﴿٧﴾ ﴾

**"Nyuso nyingine siku hiyo zitadhalilika. Zitahangaika na kusumbuka. Na zitaingia katika moto mkali. Zitanyweshwa maji ya moto yachemkayo. Na hawatakuwa na chakula isipokuwa miiba, chakula hicho hakinenepeshi wala kuondoa njaa". Surat Al-Ghashiya, aya ya 2-7.**

Halikadhalika akasema katika Aya nyengine kuhusu nyuso za wema na waovu*:*

﴿ وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ مُّسْفِرَةٌ ﴿٣٨﴾ ضَاحِكَةٌ مُّسْتَبْشِرَةٌ ﴿٣٩﴾ وَوُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ عَلَيْهَا غَبَرَةٌ ﴿٤٠﴾
تَرْهَقُهَا قَتَرَةٌ ﴿٤١﴾ ﴾

**Nyoso siku hio zitanawiri**Zitacheka zitachangamka**Na nyuso (nyengine) siku hio zitakuwa na mavumbi juu yake**Giza totoro litazifunika". Surat Abasa 80 : aya ya 38-41.**

Watu hawa wabaya, Qur'ani haikuwaeleza kuwa wataona lolote lile bali imewaeleza kuwa wataona adhabu kali na mateso. Wala hazikueleza ya kuwa hawatamwona Mola Wao bali zimeeleza kule kukosa kwao raha na zile neema za peponi ambazo wenzao waumini watazitumia wakiwa humo na hatimaye wataziona kwa macho yao huku wakifurahia neema hizo. Na huko kusemwa *"ila rabiha nadhira"* ni jambo la majazi tu lakini maana yake hasa ni kuwa waumini hapo wameelezwa kuwa watamtazama Mola Wao kwa kumaanisha kungojea kupewa neema na malipo bora. Na hili liko wazi, kwani Aya hizi zinaelezea hali ya kisimamo cha Qiyama kabla ya wema kwenda peponi na waovu kwenda motoni. Hivyo kama tulivyotangulia

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 43



kueleza, ni kuwa kumtazama mja Mola Wake ni kusubiri kupewa neema na malipo ama Mola kumtazama mja wake kunamaanisha kumrehemu ama kumuokoa na adhabu. Na katika aya *"Wala yandhuru ilayhim"* yaani, "na wala Mwenyezi Mungu hatawatazama,"**[46]**neno *"wala yandhuru ilayhim"* halimaanishi kuwa Mwenyezi Mungu hatawaona ama hatawatazama bali linamaanisha kule kutozingatia Mwenyezi Mungu maombi ya makafiri baada ya kuingizwa motoni. Kwa dalili hizi Mwenyezi Mungu hawezi kuonekana na macho ya yeyote ni sawa hapa Duniani au Akhera, bali nyoyo ndizo zitakazozidi kumwona Mola Wao kwa maana ya kupata maarifa zaidi juu ya Mola Wao huko Akhera.

## CHIMBUKO LA ITIKADI HIZI

Itikadi hizi potofu za kuonekana kwa Allah kwa macho ya wanadamu na kuwa Allah ana kiwiliwili au ana sifa zinazofanana na wanadamu ni natija ya Hadithi kadhaa za Uongo zilizopokewa kwa jina la Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na baadhi ya watu amma kwa makusudi, kwa ujinga au kwa kutokujua natija zake mbaya zenye kupotosha itikadi na falsafa ya Dini ya Kiislamu iliyotegemea sana Tawhiid na msingi wa kumpwekesha Allah.

Kwa maelezo haya machache ya Kitabu hiki, sina nia ya kuwalaumu ndugu zangu wa Ahlul Sunnah au wale wa Kisalafi bali nina nia ya kuwazindua na kuwapatia fursa nyengine kubwa ya kuzirudia hizo Hadithi zilizotuletea mfarakano wa kiitikadi na wa kiimani ili kurekebisha mambo.

Kuna Hadithi nyingi zilizosababisha haya tunayoyasema, lakini kwa kuwa hatuwezi kuzinukuu Hadithi zote hizo, hapa tutatowa kidogo

[47] **Surat Al-Imran** aya ya 77.

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 44



mifano ya Hadithi hizo, inasikitisha kuona kuwa Hadithi kama hizo zinapatikana katika Vitabu vinavyokubaliwa kuwa ni *Sahih* na wengi wa Waislamu, hivyo katika nasaha hizi nawaomba Masheikhe na wasomi wa Dini kuzirudia Hadithi hizo na kuzitafakari bila ya kuwa na ushabiki na wazirudie Hadithi hizo kwa kuzipima na Kitabu cha Mwenyezi Mungu, hayo ndiyo yatakayopelekea kutambua usahihi wake na uhakika wa habari zilizoletwa na Hadithi hizo. Mfano wa Hadithi zilizotuletea mfarakano huu na kuweka itikadi potofu katika Uislamu juu ya Upweke na sifa za Allah ni hadithi zifuatazo:

Imam Muhammad Bin Ismail, aliye maarufu kwa jina la Imam Al-Bukhari na mwanafunzi wake aitwaye Imam Muslim Sijistani, wamepokea Hadithi iliyosimliwana Abdul-Razak, aliyeisikia kutoka kwa Ma'amar ambaye aliisikia kutoka kwa Hamma Bin Munabbih kuwa Abu Hurayra (r.a) amesema, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Muhammad (s.a.w.w.) amesema: "Allah alimuumba Adam kwa mfano wa sura Yake, urefu wake Adam ulikuwa dhiraa sitini." Mambo hayakuishia hapo lakini tunamuona Imam Ahmad Bin Hanbal naye anatupokelea Hadithi hiyo hiyo kwa sanad nyengine ya Tabi'i maarufu aitwaye Saeed Bin Mussayyib kuwa Abu Hurayra (r.a.) pia alisema kuwa "upana wa Adam ulikuwa ni dhiraa saba."

Tazama:
*Sahiih Al-Bukhari*, Juz. 4, uk. 57.
*Sahiih Muslim*, Juz. 2, uk. 481.

(iii) *Musnad Ahmad*, Juz. 2, uk. 315.

Kwa mujibu wa Hadithi hiyo, tunaambiwa kuwa Allah kamuumba Adam kwa mfano wa Sura Yake na halafu tukaambiwa kuwa Abu Hurayra alimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema kuwa Adam aliyeumbwa na Allah kwa mfano wa sura Yake alikuwa na urefu wa

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 45



dhiraa sitini na upana wa dhiraa saba! Jee, kwa mujibu wa mantiki hii ndio Maimamu hawa (Al-Bukhari, Muslim na Ahmad Bin Hanbal) wanatwambia kuwa Allah ana urefu wa dhiraa sitini na upana wa dhiraa saba? Hakika ametakasika Allah na masingizio kama haya, hakika Allah yu kama alivyoisifu Nafsi Yake na Dhati Yake kwa kusema ***"Walam yakun lahu kufuan ahad"* - Na wala Allah hana mfano wa cho chote kile kiwacho." Surat al-ikhlas**, Sura ya 112 aya ya 6. Hivyo, maneno hayo ya Hadithi ya kuwa Allah kamuumba Adam kwa mfano wa Sura Yake **HAYANA MAANA YO YOTE – BALI NI MANENO YA KIYAHUDI HAYA.** Jee haijafikia wakati wa kuitupa Hadithi hiyo na imani hiyo katika jaa au pipa la taka na kukikumbatia Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Qur'ani ambayo haina shaka wala dosari?

Kwa bahati mbaya Maulamaa wa Kisunni mpaka leo wanadai kuwa Hadithi kama hii tunayoieleza ni sahihi ijapokuwa wanajizuilia na kuzifasiri kama zilivyo, wananyamaza kimya kwenye tafsiri zake huku wakiamini usahihi wake kama walivyosema haya Imam An-Nawawi kwenye *Sherhe* yake ya *Sahiih Muslim* iliyochapwa pembezoni mwa *Sahiih Al-Bukhari*, juzuu ya 12, ukurasa wa 18. Pia unaweza kupata kukubali kwa imani kama hiyo kutoka kwa Imam Ibnu Hajjar Al-Qastalani, ukisoma kitabu chake kiitwacho *Irshad As-Sari*, juzuu ya 10, ukurasa wa 491.

Hakika kutegemea kwa Hadithi kama hizi kujenga imani au itikadi bila ya kujali matamshi ya Qur'ani juu ya Dhati ya Allah ni upotevu wa mwisho, haya na mengine ya mfano wake ndiyo yaliyopelekea kutokea kwa waislamu waliodai kuwa Allah ana viungo na kuwa anashuka kutoka mbinguni na kuwa anakaa juu ya kiti chake kama Mfalme anavyokaa juu ya Kiti chake cha ufalme! Mawazo kama haya yamewapelekea wengi kuamini kuwa Allah alikuwa na mwili ingawa mwili wake unamstahikia yeye tu, yote haya ni DHANNA na itikadi

kama hizi hazina usahihi wowote, kwa hakika Allah ni kama alivyojisifu mwenyewe kwa kusema yeye ni **"Nuru ya Mbinguni na Ardhini"** (**Surat An-Nuur**). Tunamuomba Allah atuzindue na aturejeshe kwenye Kitabu Chake na kwenye mwendo sahihi wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.), amin!

Kwa hakika hakuna haja ya kutegemea mahadithi ya uongo, Kitabu cha Mwenyezi Mungu kinatosha kutupa mwanga wa kutambua Hadithi sahihi kutoka zile za uongo, Mwenyezi Mungu ameepukana na mwili wa aina yo yote, hahitajii mwili wala viungo, hahitaji kupanda na kushuka, na huko kushuka usiku wa manane kuingia uwingu wa Dunia, anakuja kutafuta nini au kuleta nini ambacho hawezi kukiona, kukipata au kukitengeneza anapokuwa popote awako? Hizi ni dhanna za wajinga kati yetu na tunamuomba Mola atuweke kwenye Nuru yake na atuongoze kwenye mwanga wa imani sahihi, amin!

Kwa hakika Allah yu karibu na wanadamu au vyote alivyoviumba kwa ukaribu Wake unaomstahikia Yeye tu *Subhanahu wa Ta'ala* bila ya masafa, mwili au upande, ametakasika *Subhanahu wa Ta'ala* na kuhitajia masafa, upande au mahala, Yeye alikuwepo kabla ya kuwepo kwa masafa au mahala kwa kuwa Yeye ndiye Muumba wa asili wa haya yote, ametakasika Allah na yale wanayomsingizia wajinga! – Wale waliochomekea hadith kama hizo.

Imam Al-Bukhari na Imam Muslim hawakuishia hapo, bali wameendelea kupokea Hadithi zenye kumweleza Allah kwa sura nyengine kabisa ambayo haimstahikii kabisa Yeye Mwenyewe *Subhanahu wa Ta'ala*! Wamepokea Hadithi ndefu kwa sanad ya watu wale wale wa mwanzo waliotangulia akina Abdul-Razak, naye kutoka kwa Maamar, naye kutoka kwa Hammam Bin Munabih, naye kutoka kwa Abu Hurayra (r.a.) kuwa, Mtume amesema; "….Lakini moto wa jahannam hautajaa mpaka pale Allah atakapotumbukiza mguu wake

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 47



ndani ya moto huo, na hapo Jahannam itasema 'nimetosheka! Nimetosheka! Hapo ndipo jahannam itakapojaa na sehemu zake zote kuungana"

Tazama:
(i) *Sahiih Al-Bukhari*, Juz. 3, uk. 127
(ii) *Sahiih Muslim*, Juz. 2, uk. 482;
(iii) *Musnad Ahmad Bin Hanbal*, Juz. 2, uk. 314.

Jamani, ni kwa vipi Allah anaweka mguu Wake kwenye Jahannam? Jee, Allah yuko na miguu? Haya ndiyo tunayoyasema, wenzetu mpaka leo hawajatambua hasa nini Tawhiid, wanadai na kuipigia sana kelele Tawhiid, lakini wapi? Wanasikia na kufahamu hiyo Tawhiid? Kwa vipi basi Kiongozi wao huyu Al-Bukhari anaikubali Hadithi kama hii? Na kwa vipi basi kwa karne zote hizi wameweza kuisomesha Hadithi kama hii na kuwalazimisha watu kuamini kuwa Allah ataweza kufanya kitendo kama hicho Siku ya Kiyama?

Jee, haya si dhahiri haya tunayosema kuwa hawa wanaamini kuwa Allah ana viungo na mwili? Ushahidi wa haya ni hayo wanayoyasema kuwa Moto wa Jahannam hautajaa isipokuwa baada ya kuingiza Allah mguu Wake ndani yake, jee imani hii si inapingana na maneno yake Allah aliyoyasema juu ya moto wa Jahannam? Allah amesema katika Kitabu chake kuwa:

﴿ قَالَ اخْرُجْ مِنْهَا مَذْءُومًا مَّدْحُورًا ۖ لَّمَن تَبِعَكَ مِنْهُمْ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٨﴾ ﴾

**"Allah akasema, toka nje ya bustani ukiwa umelaaniwa na kutengwa na rehma zangu; na kwa ye yote atakayekufata wewe; nitaijaza Jahannam kwa miili yenu nyote" (Sura:7:18).**

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 48



Katika aya nyengine Allah anasema

﴿ إِلَّا مَن رَّحِمَ رَبُّكَ ۚ وَلِذَٰلِكَ خَلَقَهُمْ ۗ وَتَمَّتْ كَلِمَةُ رَبِّكَ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١١٩﴾ ﴾

**“Isipokuwa wale aliowarehemu Mola Wako na kwa ajili hiyo ndiyo aliwaumba; na kauli ya Mola Wako itatimia, ya kuwa nitaijaza Moto wa Jahannam kwa Majini na Wanadamu” Sura. 11:119.**

Na katika aya nyengine Allah anasema:

﴿ وَلَوْ شِئْنَا لَآتَيْنَا كُلَّ نَفْسٍ هُدَاهَا وَلَٰكِنْ حَقَّ الْقَوْلُ مِنِّي لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١٣﴾ ﴾

**“Na Laiti tungependa tungeziongoa nafsi zote, lakini kauli yangu ni ya Haki ya kuwa nitaujaza moto wa Jahannam kwa Majini na Wanadamu” Sura. 32:13.**

Je, basi sisi waislamu na waumini wa kweli tutaweza kuacha Kauli ya Allah isemayo kuwa Yeye **“Ataujaza Moto wa Jahannam kwa kutumbukiza humo Miili ya Majini na ya Wanadamu;”** na badala yake tuamini Hadithi ya Al-Bukhari na Abu Hurayra inayosema kuwa **- “Jahannam haitajaa mpaka baada ya kutumbukizwa kwa Mguu wa Allah?”**

Moto umeumbiwa watu waovu, sasa na Mwenyewe Muumbaji aingize Mguu Wake humo, je mguu huo nao ni muovu au ni wa muovu? Mwenye Macho haambiwi tazama, na mwenye akili haambiwi tafakari, huu ni ujumbe wako wewe Muumini uliyenaswa na mahubiri ya Kiwahabi na itikadi potovu zisizolingana na Qur’ani na

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 49



Sunnah sahihi. Wao wanawakufurisha waislam wengine kwa mambo wanayoyafanya, yenye mantiki katika Uislam, kwa kuyaita ni Bidaa na wanaoyafanya ni Mushrikina. Je haya yao sio ushirikina wa dhahiri, wao na waislam wengine ni nani mushrik hasa? Tafadhali ewe ndugu mtakase Allah na sifa hizo za viungo na mwili, na umpwekeshe kama anavyoagiza kupwekesha, inshaallah utakuwa umeepukana na ushirikina huu wa Kiwahabi.

Maimamu hawa wawili kama kawaida yao wanatwambia tena kuwa Allah **ANASHUKA** na **KUPANDA** baina ya **ARSHI** Yake na Uwingu wa Dunia inapobakia theluthi moja ya kila usiku, katika Hadithi iliyosimuliwa na Ibnu Shihaab naye kutoka kwa Abu Abdullah Al-Aghar na Abu Salamah Bin Abdul Rahman kuwa Abu Hurayra (r.a.) amesema; “Mola wetu hushuka kwenye Uwingu wa chini inapobakia theluthi ya mwisho ya kila usiku na (Allah) husema; ‘Yoyote anayeniomba nitamkubalia ombi lake.’

Tazama:
(i) *Sahiih Al-Bukhari*, Juz. 4, uk. 68.
(ii) *Sahiih Muslim*, Juz. 1, uk. 283.
(iii) *Musnad Ahmad*, Juz. 2, uk. 258.

Hali hii ya kupanda na kushuka kwa Allah *astagh-firullah*, ameieleza Ibnu Taymiyyah kwa kuifanya kwa vitendo hasa. Siku moja Ibnu Taymiyyah alikuwa anahutubia kule Damascus, Syria, akashuka ngazi moja juu ya Minbar yake huku anaeleza namna ya Allah anavyoshuka na kupanda kutoka juu kuja kwenye Uwingu wa Dunia! (57) *Subhanallah!* Hakika Allah ametakasika na kupanda na kushuka kama alivyojisifu kwa kusema:

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 50



﴿ وَهُوَ ٱلَّذِى فِى ٱلسَّمَآءِ إِلَٰهٌ وَفِى ٱلْأَرْضِ إِلَٰهٌ ۚ وَهُوَ ٱلْحَكِيمُ ٱلْعَلِيمُ ﴿٨٤﴾

**"Yeye Ndiye Allah Mbinguni na Allah Ardhini, naye ni Mwenye Hikma na Mwenye Kujua." Sura. 43:84.**

Sasa Allah ambaye ni Mungu Mbinguni na Ardhini kweli atahitaji kupanda na kushuka? Yeye Ndiye aliyemuona na kumwokoa Yunus akiwa kwenye Kiza cha Bahari na Kiza cha tumbo la Nyangumi, atashindwa kuwaona hao wanaoswali au wenye kumuomba Usiku mpaka pale atakaposhuka kwenye Uwingu wa Dunia?

**Kwa nyongeza:** Kuongeza zaidi ukamilishaji wa ushahidi huu ni aya nyingine ya Qur'ani ifuatayo:

﴿ أَلَمْ تَرَ أَنَّ ٱللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِى ٱلْأَرْضِ ۖ مَا يَكُونُ مِن نَّجْوَىٰ
ثَلَٰثَةٍ إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ وَلَآ أَدْنَىٰ مِن ذَٰلِكَ وَلَآ أَكْثَرَ
إِلَّا هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا۟ ۖ ثُمَّ يُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا۟ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ بِكُلِّ شَىْءٍ عَلِيمٌ ﴿٧﴾ ﴾

**"Kwani huoni kwamba Mwenyezi Mungu anajua vilivyo katika mbingu na vilivyo katika ardhi? Hauwi mnong'ono wa watu watatu ila Yeye huwa ni wanne wao, wala wa watano ila Yeye huwa ni wa sita wao. Wala wa wachache kuliko hao, wala walio wengi zaidi, ila Yeye yuko pamoja nao popote pale walipo. Kisha Siku ya Kiyama atawaambia waliyoyatenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu." 58:7**

(Ikiwa kwa aya hii, Yeye mwenyewe anathibitisha kwamba yupo kila mahali, hata alipo mtu mmoja, au wawili wanaonong'ona anawasikia, sasa anashuka kutoka wapi tena, vipi litaingia akilini hili jamani? Au aya kama hizi ndani ya Qur'ani Yake wao hawazioni? )**- Mhariri**

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 51



Hakika, tunahitaji kutafakari na kuchukua juhudi kubwa katika kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kuwa na Tawhidi sahihi, ushirikina si kuabudu waungu wengine tu, au si kuwapa sifa za kiungu wanadamu wengine tu bali hata kumsifu Allah kwa sifa ambazo ni za viumbe Vyake, huo nao ni ushirikina pia. Tuache pia kushika ile kauli inayosemwa kuwa Mtukufu Mtume alimwona Mola Wake Usiku wa Miiraj, hii si kweli na ni uongo ulio dhahiri, Mtukufu Mtume **HAKUMWONA MOLA WAKE** usiku wa Miiraj bali aliona ishara na miujiza mikubwa kutoka kwa Mola Wake kama Kitabu cha Mwenyezi Mungu kinavyoashiria ukweli huu kwa kusema:

﴿ لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَىٰ ﴿١٨﴾ ﴾

**"Hakika (Muhammad) aliona ishara nyingi kubwa kutoka kwa Mola Wake"Qur'ani Tukufu, Sura ya 53 aya ya 18.**

Hivyo, Mtume Muhammad (s.a.w.w.), **HAKUMUONA ALLAH USIKU WA MIIRAJ**, kwa haya machache, ni matumainio yangu kuwa waislamu wenzangu watafaidika sana na mawaidha haya na haya labda yatakuwa ndio sababu ya wao kuacha Ushirikina na kumsifu Allah kwa sifa asizokuwa nazo.

Mwenyezi Mungu amesema kwa mnasaba huu**:**

﴿ فَبَشِّرْ عِبَادِ ﴿١٧﴾ الَّذِينَ يَسْتَمِعُونَ الْقَوْلَ فَيَتَّبِعُونَ أَحْسَنَهُ ۚ
أُولَٰئِكَ الَّذِينَ هَدَاهُمُ اللَّهُ ۖ وَأُولَٰئِكَ هُمْ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿١٨﴾ ﴾

**"….. Basi wabashirie waja wangu ambao husikiliza maneno kisha wakuafata yaliyo mazuri zaidi, hao ndio Mwenyezi Mungu aliowaongoa na hao ndio wenye maarifa." Qur'ani Surat Zumar aya ya 17-18.**

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 52



## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia

26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba

56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira

84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali
87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili

111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
114. Iduwa ya Kumayili
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Idil Ghadiri
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 57



136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
141. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu *Fiqhi al-Sunnah*
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No1
152. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No2
153. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No3
154. Abu Huraira
156. Kati ya Alama kuu za dini ni Swala ya Jamaa
157. Mazingatio kutoka katika Qur'ani

Kuonekana kwa Allah.qxd 7/2/2011 10:47 AM Page 58



# BACK COVER

Je, Mungu ataonekana? Hili ni suala ambalo wamehitalifiana wanavyuoni wa Shia na Sunni. Kwa ujumla, wanavyuoni wote wa Shia wanakubaliana kwamba Mungu hawezi kuonekana si hapa ulimwenguni wala kesho Akhera. Ili kuliweka wazi suala hili, Sheikh wetu, Muhammad Ali Zanjibari, amelifanyia utafiti wa kina suala hili na kuweka wazi kwamba Mungu hataonekana kwa kutoa ushahidi kutoka kwenye Qur'ani na hadithi za Mtukufu Mtume s.a.w.w

Katika kuwasilisha hoja zake, mwanachuoni huyu alitumia rejea za vitabu vingi mashuhuri vikiwemo vya Kisunni. Rejea na vitabu hivyo vimeorodheshwa katika tanbihi chini ya kurasa ndani ya kitabu hiki ili msomaji aweze kuvirejelea.

Ni muhimu kufikia kila aina ya maoni katika kujaribu kuamua ukweli. Uislamu kimsingi uko dhidi ya kufuata kibubusa. Ni muhimu mtu kuelewa hoja za wale ambao hakubaliani nao. Inawezekana kusemwa kwamba wale ambao hawaelewi kabisa mtazamo wa maoni tofauti, hawaelewi kwa ukamilifu (mtazamo) wa kwao wenyewe.

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
**Alitrah Foundation**
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.alitrah.org
Katika mtandao: www.alitrah.info